# Nipashe

Alhamisi Agosti 17, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581405

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII



SUPA JACKPOT

TZS. 1,144,172,464

KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ

PIGA *150*87#




**Dola** za mauzo ya madini nje hazirudi nchini

UKURASA 2




UKURASA 11


nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com 0745 700710 LIKE & FOLLOW US


SERIKALI YAANIKA

# Sababu kukamatwa Dk. Slaa na wenzake

• **Wakili** adai Dk. Slaa anashikiliwa Mbeya; mawakili 100 kuwatetea mahakamani... *Endelea ukurasa 2*



Waziri Nape Nnauye



Dk. Willibrod Slaa



Mdude Nyagali



Wakili Boniface Mwabukusi

## YALIYOMO


UKURASA WA 4

**'AFRIKA IWEKEZE KATIKA UTAFITI MBEGU ASILIA'**

WADAU wa mbegu asili wameshauri nchi za Afrika ziwekeze katika utafiti wa...

UKURASA WA 24

MWAMUZI MKONGWE HAMDUNI:

**MAREFA WA TANZANIA NI BORA NJE, SHIDA NDANI**

MWENYEKITI wa Kamati ya Waamuzi ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF)...


## Filimbi yenye damu yaibua jambo kesi dada Bilionea Msuya

UKURASA 4



## Rais Samia afichua dosari za mabalozi

UKURASA 3


MICHEZO ROBERTINHO ATAKA 'KISHINDO' AKIANZA LIGI UK.24 KATUNI UK.6



Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongela akimjulia hali mmoja wa waandishi wa habari waliolazwa katika Hospitali ya FAME Karatu jana, baada ya kujeruhiwa na vijana wa jamii ya kimaasai wakati wakitekeleza majukumu yao ya kikazi katika kijiji cha Endulen, wilayani Ngorongoro. Kushoto ni Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, ACP Justin Masejo. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Serikali yaanika sababu za kukamatwa Slaa, wenzake

**Na Waandishi Wetu**

WIZARA ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imeeleza sababu za kukamatwa kwa watuhumiwa watatu, akiwamo Balozi Dk. Willibrod Slaa kuwa ni kuitisha maandamano ya kutaka kuipindua serikali iliyopo madarakani.

Wakati serikali ikidai hayo, mawakili wa watuhumiwa hao wamedai kuwa takribani mawakili 100 wanatarajiwa kuwatetea watakapopandishwa kizimbani.

Watuhumiwa hao na tarehe walizokamatwa kwenye mabano ni Balozi mstaafu, Dk. Slaa (Agosti 13, 2023), Wakili Boniface Mwabukusi na Kada wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo CHADEMA, Mpaluka Nyagali maarufu Mdude (Agosti 12, 2023).

Juzi Wakili wa Dk. Slaa, Dickson Matata aliieleza Nipashe kuwa alimtafuta mteja wake katika Kituo cha Polisi Mbweni na Oysterbay bila mafanikio, lakini jana alimpata katika Kituo Kikuu cha Polisi jijini Mbeya, akiwa na wenzake na alizungumza naye.

Katika taarifa yake kwa umma jana, Waziri Nape Nnauye alidai kuna baadhi ya mashirika ikiwamo yanayotetea haki za binadamu yanatoa taarifa zisizo sahihi juu ya kukamatwa watu hao. Yanadai kumetokana na kukosoa mkataba wa bandari kati ya Tanzania na Umoja wa Falme za Kiarabu, jambo ambalo si kweli.

"Moja ya taarifa za hivi punde kutoka kwa Shirika la Kimataifa la Kutetea Haki za Binadamu limefanya upotoshaji mbaya kwamba watuhumiwa walikamatwa kwa kosa la kukosoa mkataba wa bandari kati ya Tanzania na Umoja wa Falme za Kiarabu," alisema Nape.

Alisema hakuna mtu aliyekamatwa au atakayekamatwa kwa kukosoa mkataba huo au mradi, mpango, programu au sera yoyote ya serikali.

Nape alisema upotoshaji wa makusudi wa taarifa kuhusu kukamatwa kwa washukiwa wa uhalifu kunaleta maswali juu ya nia ya mashirika hayo kuhusu taarifa hiyo.

Kwa mujibu wa Nape, watuhumiwa hao ambao baadhi yao alidai walihamasisha wananchi kubeba silaha dhidi ya Jeshi la Polisi na walikamatwa ili kutuma ujumbe mzito wa kuwazuia wahalifu kufanya makosa ya jinai.

Alisema kukamatwa kwa watu hao hakuzuii uhuru wa kujieleza Tanzania, bali ni sehemu ya utekelezaji wa sheria, ili kuzuia machafuko ya kijamii yanayoweza kutokea kutokana na wito wa uasi dhidi ya serikali iliyochaguliwa kidemokrasia.

Waziri Nape alisema kuwa tangu serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan iingie madarakani Machi 2021, imekuza demokrasia, nafasi ya kiraia nchini kwa kutengua zuio la mikutano ya hadhara kwa vyama vya siasa, kuondoa kufungiwa magazeti kadhaa na televisheni za mtandaoni na kupanua uhuru wa kujieleza.

"Kwa maana hiyo, watu binafsi, makundi, jumuiya za kiraia, wanachuo, vyombo vya habari, viongozi wa dini, vyama vya siasa na taasisi wanaendelea kujadili kwa uhuru masuala ya kitaifa na kukosoa msimamo wa serikali bila vitisho wala kukamatwa," alisema.

Waziri Nape alisema vyama vya upinzani kwa sasa vinafanya mikutano ya hadhara kote nchini kwa uhuru, kukosoa mpango wa bandari na sera nyingine za serikali, jambo ambalo hawakuweza kulifanya miaka michache iliyopita kabla ya Rais Samia kuingia madarakani.

Vilevile, Waziri Nape alisema serikali itaendelea kudumisha uhuru wa kujieleza, mikusanyiko ya amani na kuruhusu mijadala ya mtandaoni na hadhara kuhusu miradi ya maendeleo ya kitaifa na masuala mengine yoyote yenye maslahi ya umma.

"Hata hivyo, haki na uhuru pia huja na wajibu kwa wengine na tunatutaka sote kutii sheria na kujiepusha na maneno hatari ya jinai na ya kizembe," alisema.

**MAWAKILI 100**

Wakati huo, Mwenyekiti wa Jopo la Mawakili wanaowatetea watuhumiwa hao, Philip Mwakilima, alisema jana kuwa zaidi ya mawakili 100 kutoka taasisi mbalimbali wanatarajiwa kuwatetea watuhumiwa hao watakapopandishwa kizimbani.

Akizungumza na waandishi wa habari jana nje ya Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Mbeya, wakili huyo alisema taarifa alizopewa ni kuwa wateja wake watafikishwa mahakamani wakati wowote.

Alisema baadhi ya mawakili hao wanatoka Chama cha Wanasheria Tanzania (TLS), Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), mawakili wa kujitegemea na mawakili kutoka vyama vya siasa.

Wakili Mwakilima alidai baadhi ya mawakili hao tayari wameshaanza kuwasili mkoani Mbeya kwa ajili ya kesi hiyo na wengine wako njiani wakitokea maeneo mbalimbali nchini.

"Mawakili wengine wanatoka CHADEMA, lakini pia tumewasiliana na James Mbatia ambaye pamoja na matatizo yaliyoko katika chama chao cha NCCR-Mageuzi, alisema mawakili wao wataungana nasi," alidai Wakili Mwakilima.

Wakili huyo pia alibainisha kuwa wateja wake walishaacha mgomo wa kula na sasa wanaendelea kula huku akisisitiza kuwa yeye mwenyewe aliwashuhudia wakinywa chai jana asubuhi.

**SHAURI JIPYA**

Wakili Jebra Kambole ambaye ni miongoni mwa mawakili wanaowatetea watuhumiwa hao, alisema wanakusudia kufungua shauri mahakamani la kuiomba mahakama ililazimishe Jeshi la Polisi na Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali kuwapeleka wateja wao mahakamani ama kuwaachia huru.

Alisema jana kuwa kwa sasa kitu chochote kinachofanyika dhidi ya wateja wao katika kituo cha polisi ni batili kwa maelezo kuwa muda wa kuendelea kuwashikilia ulishakwisha na walitakiwa wawe wamefikishwa mahakamani.

# Dola mauzo madini nje hazirudi nchini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Madini imebaini baadhi ya wafanyabiashara wanaouza madini nje ya nchi hawarejeshi fedha za mauzo kwenye benki za nchini kama sheria inavyotaka hali inayosababisha upungufu wa fedha za kigeni.

Kutokana na hali hiyo, serikali imeunda kamati ya watu tisa itakayofanya tathmini ili kujua sababu za fedha hizo kutorejeshwa nchini.

Waziri wa Madini, Dk. Doto Biteko, aliyasema hayo jana jijini hapa kwenye kikao cha wafanyabiashara wa madini kilichokuwa na lengo la kujadili mwenendo wa biashara ya madini yanayouzwa nje ya nchi.

"Mfano tunajua katika mwaka wa fedha wa 2022/23 wafanyabiashara wa madini kupitia kampuni zao walisafirisha nje ya nchi madini yenye thamani ya Dola za Marekani 952,926,784. Sasa hebu tujihoji ni kiasi gani cha fedha hizo kilirejeshwa katika akaunti zenu za benki za hapa nchini?" alihoji.

"Kifungu cha 10 cha Sheria ya The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereigneity) Act, 2017, kinawataka wafanyabiashara wa madini nchini kurejesha fedha zote za mauzo ya madini katika akaunti zenu zilizoko katika benki za hapa nchini na kanuni ya 7 (1), (4) ya Foreign Exchange Regulations, 2022 inasisitiza kurejesha nchini fedha za mauzo ya bidhaa na huduma zinazouzwa nje ya nchini," alifafanua.

Alisema Wizara ya Madini ingependa kuona fedha za mauzo ya madini zinarejeshwa nchini kama sheria inavyoelekeza na kusisitiza kuwa nia ya serikali si kuingilia matumizi ya fedha zao bali inachotaka ni kuongeza mchango wa fedha za kigeni unaotokana na shughuli za madini ikiwemo biashara ya madini kupitia mifumo rasmi ya kibenki.

Biteko alisema wizara itaendelea kuimarisha usimamizi na kuweka mazingira wezeshi kwa wafanyabiashara wa madini ili kuongeza mchango wa sekta katika upatikanaji wa fedha za kigeni nchini.

Pia alisema wizara imeandaa mpango mkakati wa kuongeza mauzo ya madini nje ya nchi ambao utahakikisha kuwa sekta ya madini inaendelea kuwa ni miongoni mwa sekta zinazochangia kwa kiasi kikubwa katika kuingiza fedha za kigeni nchini.

Alisema mwaka 2022 madini yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 3,395.3 yaliuzwa nje ya nchi sawa na asilimia 56 ya mauzo yote ya bidhaa nje ya nchi sawa na ongezeko la asilimia tisa ikilinganishwa na mauzo ya Dola za Marekani milioni 3,116.40 mwaka 2021.

HABARI KITAIFA

# Samia afichua dosari za mabalozi

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan (pichani), amefichua kasoro mbalimbali za mabalozi wanaowakilisha Tanzania katika nchi mbalimbali huku akiwataka kufanya kazi kuzingatia matokeo badala ya kusubiri matukio.

Amefunguka kutofurahishwa na mmoja wa balozi ambaye vitendo vyake vilisababisha mkuu wa nchi ndani ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) (bila kuitaja) kuomba mwakilishi huyo aondolewe nchini mwake.

Katika hafla ya kuwaapisha mabalozi wapya wateule iliyofanyika jana Ikulu, Chamwino jijini Dodoma, Rais Samia alisema mkuu wa nchi hiyo alimweleza namna mwakilishi huyo haonekani kazini, hashiriki mikutano na kwamba hawamwelewi.

"Novemba, mwaka jana, nilikutana na mabalozi Zanzibar na tulizungumza mengi nadhani tukapeana majukumu au tulitoka na maazimio ambayo mpaka sasa sijaona utekelezaji au mikakati ya mabalozi kwamba amejipangaje na mpango wake ukoje?.

"Katika nchi zingine mabalozi wetu sijui niseme hawajui wanachokifanya. Nilishakutana na Rais mwenzangu ndani ya SADC akaniambia 'nibadilishie balozi, uliyeniletea hata kazini haendi, mikutano hashiriki, yupo yupo tu hatuelewi. Tanzania hatujazoea hivyo, sasa labda umbadilishe' nikamwambia nimekusikia.

"Lakini mabalozi wengine unawaona pale ambapo ujumbe wa Tanzania umekwenda kwenye nchi hiyo. Anapokea wageni anawasindikiza, au unamwona siku za sherehe za kitaifa za nchi hiyo anakwenda kuwakilisha nchi yake, lakini wengine hakuna taarifa zenye manufaa.

"Hakuna la maana linalotoka huko au labda watanzania wafanye ukorofi wakamatwe ndo utaona ripoti ya balozi lakini kwa kawaida huoni kinachokuja.

"Inawezekana pia na aina ya mabalozi tunaopeleka, kama mnakumbuka hivi karibuni nilitengeneza kamati ipitie wizara hii (Wizara ya Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki) iniletee kasoro zilizopo, mazuri yaliyopo, wapi turekebishe, nini kifanyike vipi na ugawaji wa mabalozi," alisema.

Rais alisema tayari ameshapokea rasimu ya kwanza na kuwarudishia kwa kuwaeleza baadhi ya mambo ambayo hayamo na wanaendelea kufanyia kazi. Alisema ana imani ripoti hiyo itakapokuja, itasaidia kurekebisha wizara hiyo.

Pia alisema wamekuwa wakitia saini mikataba mbalimbali ya makubaliano na nchi mbalimbali lakini mingi imebaki kabatini hawajui mwelekeo wake na utekelezaji unakwendaje.

"Atakapokuja mtu fulani kutoka hiyo nchi anasema, 'mwaka fulani tulisaini MoU (makubaliano) ilifikia hapa, bado hapa, hatujafanya hapa, miaka imepita MoU haijafanyiwa kazi kwa hiyo hizo nazo mwangalie. Tumesaini nini na tumefikia wapi, ili mkienda mjue mna kitu cha kusema," alieleza.

Rais Samia aliwakumbusha kwamba katika maeneo wanayokwenda kuwakilisha kikanda na kimataifa, maneno watakayosema ndiyo msimamo wa Rais na taifa.

"Mkifanya kinyume hayo ni yako au matendo yako yatalifaidisha taifa letu au kulifedhehesha taifa letu, ninaomba mwende mkiwa vizuri," alisema.

Rais Samia aliwaeleza mabalozi hao kuwa mchakato wao ulipitia uteuzi mkali na panga pangua nyingi kwa lengo la kuhakikisha zinazingatia mabadiliko ya hali halisi yanayotokea duniani kwa sasa yakiwamo ya sayansi za dunia na mawanda mapya ya ushirikiano.

Alisema hawana budi mahitaji ya nchi kuzingatia mwelekeo uliopo duniani kisiasa, kiuchumi, kijamii, kiulinzi na kiusalama.

Katika miaka ya hivi karibuni, alisema kumetokea mahitaji mapya ya dunia, baadhi ni mabadiliko ya tabianchi, mapinduzi ya nne ya viwanda, matumizi ya akili bandia, uchumi wa buluu, umuhimu wa madini ya kimkakati, utalii endelevu, mahitaji ya diaspora na masuala ya haki za binadamu.

"Mahitaji yote haya yanaibua fursa na changamoto kwa nchi yoyote ile. Kwa hiyo mwende mkiwa mnayajua hayo, ni vema wizara, waziri mkaainisha majukumu, wajibu na stahili za kila balozi ili kulinda maslahi yetu kwenye maeneo hayo," alisema.

Pia alisema mahitaji yao na siasa kikanda ulimwenguni ndizo zinazoamua kidiplomasia na bila kuzingatia hayo ni sawa na chama cha siasa kisichokuwa na dira wala ajenda bali kinaendeshwa na matukio.

"Sisi mabalozi hatuendi hivyo, tunakwenda kwa kujua mwelekeo wetu Tanzania ni kitu gani. Ni vyema wizara ikaainisha majukumu, wajibu na aina ya kila balozi.

"Lazima tukubali siyo kila balozi zina fursa za kupata mikopo ya bei nafuu, biashara na uwekezaji nyingine ni wajibu wao mkubwa ni kutetea nchi yetu, nisisitize mafunzo watakayopatiwa mhakikishe yasiwe ya jumla jumla," alisema.

Rais Samia alisema miaka ya 60 na 70 nchi za Bara la Asia zilikuwa na uchumi unaolingana, lakini wengine wameipita Tanzania na kutolea mfano nchi ya Thailand, kwa miaka hiyo ilikuwa na kipato cha mtu kwa mwaka (GDP per capital) Dola 166 na Tanzania 165 la sasa wamefikia Dola 7,495 na Tanzania 1,227.

Alitaka wanaokwenda upande huo, waseme wenzao wametumia uchawi gani kwenda haraka na Tanzania inakosa nini.

Rais Samia alisema pamoja na kwamba Tanzania imezidi nchi hizo katika eneo la madini, ardhi, ukanda wa bahari na maziwa lakini nchi hizo zimeizidi Tanzania katika ukuaji wa uchumi.

Aliwaeleza kuwa ni jukumu lao kutoa ushauri na mapendekezo ili Tanzania ipige hatua kiuchumi na kuboresha hali ya watanzania.

Pia Rais ameielekeza Ofisi ya Waziri Mkuu kuhakikisha Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki inaandaliwa mfumo utakaoingiza maelekezo ya ziara za viongozi wa ndani na nje ya nchi.

Alisema mfumo huo utaonyesha jukumu la kila wizara kwenye makubaliano yaliyofikiwa ili kuweza kupima utekelezaji wa makubaliano yaliyofikiwa.

Pia amewataka waibue masuala ya ushirikiano na kutafuta fursa mbalimbali ikiwamo katika sekta ya uwekezaji, utalii pamoja na mahitaji ya 'diaspora'.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, aliwaeleza kuwa watanzania wana matumaini nao na kuwataka wakaimarishe uhusiano na mataifa hayo kwa kuhakikisha diplomasia ya kisiasa, kiuchumi inaimarika.




**KOROSHO COOPERATIVE JOINT ENTERPRISE LIMITED (KCJE LTD)**

**TANGAZO LA ZABUNI**

**LOTI NAMBA 1: VIUATILIFU /KCJE/ 2024**
**LOTI NAMBA 2: MAGUNIA /KCJE/2024**

**Tarehe: 17/08/2023**

1. Vyama Vikuu vya Ushirika vinavyohudumia wakulima wa zao la Korosho vya **TANECU LTD, MAMCU, TAMCU LTD, RUNALI LTD, CORECU LTD, na LINDI MWAMBAO LTD** vinatangaza Zabuni ya Ununuzi wa pamoja wa viuatilifu na magunia kwa ajiri ya msimu wa 2024/2025.

2. Kwa idhini ya Bodi ya Vyama Vikuu hivyo, Mwenyekiti wa Bodi ya Korosho Cooperative Joint Enterprise anawatangazia Wazabuni wote ambao wana uwezo wa kusambaza Viuatilifu vya zao la korosho na Magunia kuwasilisha maombi yao.

3. Mzabuni mmoja anaruhusiwa kuomba Loti zaidi ya moja au sehemu ya Loti kulingana na uwezo alionao. Nyaraka za zabuni zinapatikana kwa malipo ya shilingi laki tano tu (Sh. 500,000/=) malipo hayo yapitie kwenye :-

   **AKAUNTI NAMBA: 0150771321300**
   **JINA LA AKAUNTI: KOROSHO COOPERATIVE JOINT ENTERPRISE LTD**
   **BENKI: CRDB – TAWI LA MTWARA**

4. Mchakato wa zabuni hii utafanyika kwa njia shindani ya Kitaifa ( NCT) kwa mujibu wa kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 na marekebisho yake ya mwaka 2016 na ni zabuni ya wazi kwa wazabuni wote wenye sifa stahiki.

5. Wazabuni wote wanakaribishwa ofisi ya Katibu wa Korosho Cooperative Joint Enterprise iliyoko Mtwara mjini mtaa wa MADUKA MAKUBWA Jengo la Ushirika wa TANECU LTD ghorofa ya kwanza kwa ajili ya kuwasilisha maombi. Muda wa kuwasilisha ni saa za kazi kuanzia saa mbili asubuhi (2:00) hadi saa kumi na nusu jioni (10.30) isipokuwa siku za Jumamosi na Jumapili pamoja na siku za siku kuu.

6. Wazabuni wote wawasilishe zabuni zao katika Nakala tatu (nakala halisi moja, na nakala kivuli mbili) zikiwa zimefungwa kwa umakini na kuwekwa lakiri. Zabuni zote zitafunguliwa mara baada ya muda wa mwisho wa kuwasilisha. Tukio ambalo litakuwa la wazi kwa wazabuni na wawakilishi wao pia wanakaribishwa kuhudhuria. Mwisho wa kupokea ni tarehe 06/09/2023 saa nne asubuhi (4:00) katika chumba cha mikutano TANECU LTD Mjini Mtwara.

   **Maombi yatumwe kwa Anuani ifuatavyo:-**
   **Mwenyekiti wa Bodi,**
   **Korosho Cooperative Joint Enterprise Ltd**
   **S.L.P. 660**
   **MTWARA.**

7. Zabuni zote zitakazochelewa hazitafikiriwa wakati wa tathimini bila kujali sababu zozote za kuchelewa.

8. Zabuni zitakazotumwa kwa email, telegram au fax hazitafunguliwa na kufanyiwa kazi.

**IMETOLEWA NA:**
**MWENYEKITI WA BODI**
**KOROSHO COOPERATIVE JOINT ENTERPRISE LIMITED**

217554801



Mkurugenzi wa Mgahawa wa chakula Ostadhi Food Restaurant, Radhia Daffa akikabidhi msaada wa vitu mbalimbali vikiwemo vyakula vyenye thamani ya Sh, milioni moja kwa shule ya wanafunzi wasioona na matatizo mbalimbali, wilayani Same, mkoani Kilimanjaro juzi, ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan katika programu ya Tabasamu na Mama. **PICHA: ASHRACK MIRAJI**

# Filimbi yenye damu yazua jambo kesi mauaji dada Bilionea Msuya

**Na Grace Gurisha**

MKEMIA Dk. Fidelis Segumba ameieleza mahakama kuwa hajui damu ya binadamu iliyokutwa kwenye filimbi ya chuma inayodhaniwa kuwa ilikuwa inatumiwa na marehemu Aneth Msuya kuwa ilikuwa ya binadamu wangapi.

Aneth ambaye ni mdogo wa aliyekuwa mfanyabiashara wa madini mkoani Arusha, Erasto Msuya, maarufu kama Bilionea Msuya (sasa marehemu), aliuawa Mei 25, 2016 kwa kuchinjwa shingoni nyumbani kwake, Kibada, Kigamboni mkoani Dar es Salaam.

Dk. Segumba ambaye ni Meneja wa Maabara ya Sayansi Jinai Kemia katika Mamlaka ya Mkeamia Mkuu wa Serikali, alidai hayo jana mbele ya Jaji Edwin Kakolaki wakati akijibu maswali ya dodoso kutoka kwa Wakili wa Utetezi, Peter Kibatala.

Dk. Segumba alidai kuwa damu iliyokuwa kwenye vielelezo hawezi kusema ilikuwa ya Aneth au la bali jibu lake hajui kama ni damu ya marehemu. Ifuatayo ni sehemu ya majibu ya Dk. Segumba kama alivyohojiwa na Kibatala:

**Kibatala:** Katika ukurasa wa pili wa ripoti yako, umesema uchunguzi wa awali umedhihirisha kuwa kuna damu ya binadamu. Unafahamu zilikuwa damu za watu wangapi?

**Shahidi:** Jibu langu kielelezo kilikuwa na damu.

**Kibatala:** Swali langu ni damu ya watu wangapi?

**Shahidi:** Ili kujua ni damu ya watu wangapi lazima turudi kwenye jedwali la ripoti yangu ya vinasaba.

**Kibatala:** Mheshimiwa Jaji naomba anijibu swali langu liko wazi kabisa, kwamba ni damu ya watu wangapi?

**Shahidi:** Siwezi kujua.

**Kibatala:** Ni sampuli gani iliyoletwa kupima kutoka kwa mshtakiwa wa pili (Revocatus Muyela)?

**Shahidi:** Mpanguso kutoka ndani ya mashavu yake.

**Kibatala:** Ooh nilitaka kujua kama ulipima damu yake.

**Shahidi:** Akatabasamu

**Kibatala:** Umesema kwenye uchunguzi wako jinsi inaonyesha kinamilikiwa na jinsi mbili una maana gani?

**Shahidi:** Maana yake ni kwamba kielelezo hiki kina jinsi ya kiume na jinsi ya kike.

**Kibatala:** Kwenye kielelezo C, filimbi ya chuma ambayo inadhaniwa kuwa ilikuwa inatumiwa na marehemu Aneth pia umeyapata kwenye barua uliletewa?

**Shahidi:** Ndio maana yake.

**Kibatala:** Huyu mmiliki mwenye jinsi ya kike wewe unamfahamu?

**Shahidi:** Nizungumze kwa ujumla wake kwamba kwenye vielelezo vyote hakuna ninayemfahamu.

**Kibatala:** Kwenye kipengele B chupi ya rangi ya zambarau ulisema uchunguzi ulionyesha umiliki wa jinsi mbili, chanzo kilikuwa nini?

**Shahidi:** Kwangu chanzo ni chupi inayodhaniwa alikuwa ameivaa marehemu Aneth Msuya na kuvuliwa kwa nguvu.

**Kibatala:** Kwa kuwa uchambuzi wako unonyesha 'genetic profile' mbili ya kiume na ya kike huwezi kuona kuwa chanzo ni huyo binti kujamiiana na mtu mwingine kabla ya tukio?

**Shahidi:** Kwa uchunguzi nilioufanya mimi siko katika nafasi ya kusema hilo ni kweli au la.

**Kibatala:** Pia huwezi kusema kwamba hiyo chupi ilivuliwa kwa nguvu kama ile barua ya maombi ya uchunguzi iliyoletwa ilivyosema. Huwezi kujua ilivuliwa kwa nguvu katika tendo gani? Wakati wa kuuawa au wakati anafanya tendo la ndoa?

**Shahidi:** Hilo siwezi kusema.

**Kibatala:** Wala huwezi kusema kwa hakika kuwa hizo 'genetic profile' mbili ziliingia kwa wakati mmoja au kwa nyakati tofauti?

**Shahidi:** Kwa uchunguzi wangu siwezi kuamua hilo.

**Kibatala:** Wakati unatoa ushahidi wako hapa jana ulisema hujui 'force number' ya ofisa yeyote aliyeleta hizo sampuli kwako. Ni sahihi?

**Shahidi:** Kwa kweli sikumbuki.

**Kibatala:** Katika ripoti yako utangulizi unasema ulipokea kifurushi kilichofungwa kwa lakiri, unafahamu kwa nini kilifungwa kwa lakiri?

**Shahidi:** Nafahamu.

**Kibatala:** Mwambie Jaji kwa nini?

**Shahidi:** Ni utaratibu sampuli zinazoletwa maabara kuwa katika hali ambayo si rahisi kuwa tempered (kuharibiwa).

**Kibatala:** Ulitoa hapa mahakamani hiyo bahasha iliyotoka maabara ili mahakama ijiridhishe kwamba hicho kifurushi kilikuja kwako kikiwa kimefungwa? Kwa sababu sheria inaelekeza.

**Shahidi:** Ndiyo hivyo nilivyopokea baada ya uchunguzi nikavifunga tena ndiyo niliyoitoa jana.

**Kibatala:** Wakati unavifunga ulikuwa na mtu mwingine kuhakikisha kuwa umevifunga?

**Shahidi:** Hapana.

**Kibatala:** Uliifafanulia mahakama kuwa wakati unapokea na kuvifunga ulikuwa peke yako?

**Shahidi:** Ndiyo.

Washitakiwa katika kesi hiyo namba 103 ya mwaka 2018 ni mke wa Bilionea Msuya, Miriam Mrita na mfanyabiashara Revocatus Muyela, wote wakazi wa Arusha.

# 'Afrika iwekeze katika utafiti wa mbegu asilia'

**Na Mwandishi Wetu**

WADAU wa mbegu asili wameshauri nchi za Afrika ziwekeze katika utafiti wa mbegu asili kwa kuwa zina lishe bora, uhakika wa chakula na salama kwa afya ya mtumiaji.

Wadau hao kutoka nchi 25 za Bara la Afrika, Marekani na Ulaya wanakutana jijini Dar es Salaam kwa siku tatu kujadili hatma ya mbegu asili katika nchi zao na dunia kwa ujumla.

Katika mkutano huo, Paul Chilewa kutoka Mwamvuli wa Asasi za Kuendeleza Kilimo Hai Tanzania (TOAM), alisema mkutano huo ambao umehusisha zaidi ya watu 100 kutoka nchi 25 ni muhimu kwa wadau wote wa mbegu asili kujadiliana namna ya kuzilinda mbegu za asili.

Chilewa alisema Afrika kwa sasa ina changamoto kubwa ya mbegu za asili, hali itachangia kukosekana uhakika wa chakula kwa siku nyingi.

"Mbegu asili zina lishe nyingi na salama kwa afya ya mtumiaji, hivyo ili kuhakikisha zinakuwa endelevu, ni lazima kufanyika utafiti ambao utaonesha ni namna gani tunaweza kuzilinda," alisema.

Ofisa huyo alisema iwapo serikali itafanya utafiti ambao utashirikisha wakulima ambao wanatumia mbegu asili, ni wazi changamoto hiyo itapata jibu sahihi.

Chilewa alisema iwapo hakutokuwa na juhudi za kukabiliana na changamoto ya mbegu asili, ni wazi kuwa wakulima watataingia katika mtego wa kununua mbegu ambazo zitahitaji viuatilifu na mbolea, vitu ambavyo vina sumu na kusababisha maradhi mbalimbali.

Mratibu wa Mtandao Baionoai Tanzania (TABIO), Abdallah Mkindi alisema utafiti unaonesha asilimia 80 ya wakulima wa Afrika wanatumia mbegu asili, hivyo ni muhimu kuhamasisha matumizi ya mbegu hizo.

Alisema utafiti pia umeonesha mbegu asili zina virutubisho, hivyo iwapo jamii itahamasishwa kutumia, changamoto ya utapiamlo ambayo inakabili mataifa hayo itapatiwa suluhisho.

"Mbegu asili zina nafasi kubwa ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ambayo yameonesha madhara makubwa duniani, hivyo rai yangu ni kuziomba serikali za Afrika kutenga fedha zitakazotumika kufanya utafiti wa mbegu hizi," alisema.

Mkindi alisema TABIO kwa kushirikiana Mtandao wa Uhuru wa Chakula Dunia (AFSA) na SwissAid wamewakutanisha wadau hao, ili wajadiliane na kutoka na kauli moja kuhusu hatima ya mbegu asili ambazo zinaonekana kupewa kisogo na watunga sera na sheria.

Mbunge wa Lindi Mjini, Hamisa Abdallah, alisema kilimo cha mbegu asili kinaweza kuleta tija katika sekta hiyo, kwa kuwa historia inaonesha wazee wa zamani walitumia njia hiyo.

Hamida alisema mbegu asili hazina gharama katika kilimo kama ilivyo kilimo cha kisasa, hivyo ni wakati mwafaka jamii kurejea katika mfumo huo wa zamani.

Alisema kutokana na madhara ambayo yanapatikana kwenye kilimo cha kisasa, dunia imeanza kubadilika na kutaka kurejea mifumo ya zamani ambayo ilijikita katika mbegu za asili.

"Sisi Lindi tumefungua benki ya mbegu asili, hiyo ikiwa ni kuonesha ni namna gani tumejipanga kuachana na mbegu za kisasa ambazo zina madhara mengi kwenye afya ya binadamu," alisema.

Mwakilishi wa Wizara ya Kilimo, Beatrice Banzi, alisema Tanzania imekuwa ikihamasisha watafiti kufanya utafiti katika sekta hiyo ya mbegu asili na mbegu zingine.

Alisema kilio cha dunia ni uhaba wa mbegu bora na salama kwa afya ya binadamu, hivyo utafiti pekee ndiyo unaweza kutoa jibu.

Ofisa Program wa AFSA, Famara Diédhiou alisema ni wakati mwafaka kwa nchi za Afrika kuungana kuhakikisha mbegu asili zinapewa kipaumbele katika sekta ya kilimo.

Nchi zilizoshiriki ni Tanzania, Kenya, Uganda, Ethiopia, Senegali, Burkina Faso, Ivory Cost, Hispania, Norway, Zambia, Zimbabwe, Australia, Togo, Mali, Benin, Chad, Tunisia, Niger, Afrika Kusini, Botswana, Malawi, Misri, Rwanda, DR Congo na Gabon.

HABARI KITAIFA

# Tanzania yaridhishwa ushirikiano wake na India

**Na Romana Mallya**

WAKATI India ikisherehekea miaka 77 ya Uhuru wake, Tanzania yaeleza namna ilivyonufaika katika sekta mbalimbali kupitia ushirikiano wake na nchi hiyo.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, aliyasema hayo juzi mkoani Dar es Salaam katika maadhimisho yaliyoandaliwa na Ubalozi wa India Nchini kwa kushirikiana na Kituo cha Utamaduni wa India Swami Vivekananda (SVCC).

Sherehe hizo zilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wakiwamo mawaziri, wabunge, mabalozi wanaowakilisha nchi zao nchini, diaspora wa India waishio Tanzania na wahariri kutoka vyombo vya habari mbalimbali.

"Nchi hizi mbili Tanzania na India zimekuwa na urafiki wa muda mrefu, hususani serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

"Tunashukuru mikopo iliyotolewa na serikali ya India kupitia Benki ya Exim inayohusu miradi mikubwa ya maji katika miji 24 wa jumla ya Dola za Kimarekani milioni 500.

"Maji haya yakipatikana yatasaidia watanzania wasiopungua watu milioni sita ambao watanufaika kwa kupata maji safi na salama," alisema.

Kadhalika, alizungumzia mpango wa kuendelea kushirikiana kwenye kutoa elimu kwa makundi ya vijana na watumishi wa umma kupitia program mbalimbali zinazotolewa na taasisi za India, vikiwamo vituo vya ushirikiano wa utamaduni na kiuchumi.

Alisema ushirikiano huo wa kupeana ujuzi na elimu unasaidia kujenga jamii hasa katika masuala yanayohusu teknolojia za mawasiliano na nyingine.

"Tukizingatia kwamba wenzetu kule India wako hatua ya mbele zaidi kwenye mpango wa teknolojia. Tunawashukuru na tunaomba programu hii iendelee.

"Tunafahamu hivi karibuni Waziri wa Afya, (Ummy Mwalimu) alifanya ziara na miongoni mwa mambo makubwa aliyoyafanya akiwa India ni kukutana na viongozi wa hospitali kubwa na maarufu ya Apollo na BLK ambazo amezishawishi kuja kuwekeza Tanzania," alisema.

Waziri Ulega alisema taarifa walizonazo hospitali hizi na taasisi nchini humo, zimeonesha utayari wa kuja kuwekeza Tanzania.

Hata hivyo, kiongozi huyo alisema Tanzania kuna changamoto ya uzalishaji wa dawa kwa ajili ya binadamu na zikiwamo za wanyama.

"India imewekeza vizuri kupitia taasisi ya sekta binafsi upande wa mifugo, kipo kiwanda cha kutengeneza chanjo chenye asili ya India hapa nchini ni kikubwa na kizuri na cha mfano Afrika Mashariki, ambacho kinahakikisha tunapata chanjo kwa ajili ya kuhudumia mifugo," alisema.

Waziri Ulega alitaja eneo lingine ni uwekezaji unaofanywa na sekta binafsi na biashara zinazofanyika kati ya nchi hizo mbili.

Alisema India ni moja ya nchi tano zinazoongoza kwa uwekezaji nchini kwa kuwa na miradi 630 yenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 3.74 (sawa na Sh. trilioni nane), iliyotoa ajira kwa vijana na wanawake, wasiopungua 60,000. Balozi wa India Nchini, Binaya Pradhan, alisema India imetoa mikopo ya masharti nafuu ya Dola za Marekani bilioni moja kwa ajili ya kuendeleza miradi ya maji ambapo mwezi Juni, 2022, kampuni sita zilisaini ujenzi wa miradi ya maji yenye thamani ya Dola milioni 500 kwenye miji 28.

Alisema katika eneo la uwekezaji, wameona wawekezaji wengi kutoka India wakiwekeza Tanzania katika maeneo tofauti yakiwamo sekta ya usindikaji, umeme, afya, kilimo na TEHAMA.

Balozi Pradhan alisema India inatarajia kuanzisha Taasisi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) visiwani Zanzibar ambacho kitazalisha wahandisi wabobevu katika sekta hiyo.

Kuhusu uhusiano kati ya nchi hizo, alisema umeendelea kuimarika siku hadi siku na kumekuwa na ziara za viongozi wenye hadhi ya juu wakiwamo mawaziri kutembeleana.

## Baba kizimbani mashtaka ya kumnajisi mwanawe

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MKAZI wa Mtaa wa Nyabubele Kata ya Kasamwa Kukailwa (40), amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Geita kwa mashtaka ya kunajisi mwanawe - msichana mwenye miaka 14.

Alipandishwa kizimbani jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Johari Kijuwile na aliposomewa mashtaka, alikana kuhusika na kosa hilo na yuko mahabusu katika Gereza la Wilaya ya Geita baada ya kukosa wadhamini.

Upande wa Mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali Venance Mkonongo, ulidai mahakamani huko upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na kuomba tarehe nyingine kwa ajili ya kumsomea mshtakiwa maelezo ya awali.

Hakimu Mkazi Mwandamizi Kijuwile alikubaliana na ombi hilo na kuahirisha kesi hiyo hadi Agosti 30 mwaka huu kwa ajili ya kumsomea mshtakiwa huyo maelezo ya awali.

Hakimu huyo pia alitaja masharti ya dhamana kwa mshtakiwa huyo - awe na wadhamini wawili wenye barua ya utambulisho kutoka kwa Ofisa Mtendaji wa Kata na mali isiyohamishika yenye thamani ya Sh. milioni tano.

Akisoma hati ya mashtaka, Wakili wa Serikali Venance Mkonongo, alidai mahakamani huko kuwa katika tarehe tofauti Februari na Machi mwaka huu, katika mtaa wa Nyakubele, Kata ya Kasamwa, mkoani Geita, mshtakiwa alimnajisi mwanawe wa kuzaa (kulala na maharimu) - msichana mwenye umri wa miaka 14.


Coca-Cola

## BONITE BOTTLERS LIMITED

Coca-Cola

## Advertisements of Employment

1. **Mechanical Technician**
   **Qualification:**
   - Applicant should be a holder of VETA level III/Diploma in Mechanical Engineering from a recognised Institution. Form four pass in all subjects in single attempt.

   **Key skills & Abilities:**
   - Ability to maintain and troubleshooting all the mechanical equipment to acceptable and approved standards for efficient operation and to ensure smooth running of the line and service equipment by close communication with other staff.
   - Ability to operate machines as directed and to ensure they are running smoothly, efficiently and kept clean as required.
   - Able to work independently with minimum supervision
   - Self motivated, flexible person and a good team player.
   - Compliance to safety requirement at work place
   - Desire to learn and acquire more knowledge and skills.

2. **Electrical Technician**
   **Qualification:**
   - Applicant should be a holder of VETA level III/Diploma in Electrical Engineering from a recognised Institution.

   **Key skills & Abilities:**
   - Ability to maintain all the electrical equipment to acceptable and approved standards for efficient operation, and to ensure the smooth running of the line and service equipment by close communication with other staff.
   - Hanson on handling electrical circuit, PLC, knowledge of ethernet and profibus communication
   - Ability to ensure the correct electrical functioning of electrically operated equipments on the premises.
   - Able to work independently with minimum supervision
   - Self motivated, flexible person and a good team player.
   - Compliance to safety requirement at work place

3. **Plumber**
   **Qualification:**
   - Applicant should be a holder of VETA level III/ Diploma in Plumbing and pipe fitting from a recognised Institution.

   **Key skills & Abilities:**
   - Ability to assemble pipe sections, tubing and fittings
   - Ability to fill pipes or plumbing fixtures with water
   - Able to work independently with minimum supervision
   - Self motivated, flexible person and a good team player.
   - Compliance to safety requirement at work place

√ **Experience:**Six months and above in Mechanical/Electrical/Plumber field
√ **Location:** Moshi.

**Mode of Application:**
All applications accompanied with cover letter, photocopies of certificates and CVs to be sent to the undersigned, to reach him not later than 24/08/2023.

**The ManagingDirector,**
**Bonite Bottlers Ltd,**
**P.O.Box 1352,**
**MOSHI.**

217554502

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wazo la RC kufungwa kamera shuleni vyema liungwe mkono

**MIEZI** kadhaa iliyopita, serikali ilitoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya elimu yakiwamo madarasa na majengo ya utawala kwa shule za sekondari nchini ili kuhakikisha wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha tano, kuripoti mwishoni mwa wiki iliyopita bila matatizo.

Kwa ujumla, jitihada kubwa zimefanyika kwa sababu shule nyingi, hususan zile zinazopokea wanafunzi wa kidato cha tano na cha sita pekee katika tahasusi mbalimbali, zimeshamaliza kazi hiyo na kama kuna ambazo zimebaki basi ni chache na ziko katika mchakato wa umaliziaji. Kutokana na kukamilika kwa kazi hiyo, wanafunzi wameanza kumiminika kwenye shule walizochaguliwa ili kuanza masomo ya ngazi hiyo ambayo ni mlango wa kujiunga na elimu ya juu katika vyuo mbalimbali nchini.

Kutokana na kukamilika kwa kazi hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, amekwenda mbali zaidi kutaka shule zilizopewa fedha kwa ajili ya ujenzi huo, sasa kugeukia ulinzi wa wanafunzi hasa katika suala la mmomonyoko wa maadili.

Katika kupambana na tatizo hilo, Mtaka aliagiza juzi wakati wa ziara yake katika shule ya Sekondari ya Yakobi kwamba shule zilizopewa fedha sasa zifunge kamera za ulinzi (CCTV camera) kwa ajili ya kuimarisha ulinzi na kukabiliana na mmomonyoko wa maadili ambao umekuwa ukiota mizizi kila uchao katika shule nchini.

Mtaka katika agizo hilo, alisema kutokana na kuwapo kwa historia ya ukiukwaji wa maadili ulioripotiwa shuleni hapo, sasa ni wakati mwafaka kwa Mkurugenzi wa halmashauri ya Mji wa Njombe kufunga kamera hizo kuwanasa walimu ambao wamekuwa wakituhumiwa kujihusisha na matendo hayo. Alimwagiza mkurugenzi huyo kuwatuma wataalamu wa teknolojia ya Habari na mawasiliano (TEHAMA) kufanya kazi hizo kwa haraka.

Bila kuuma maneno, RC Mtaka alisema vitendo vinavyohusiana na mmomonyoko wa maadili vimetamalaki sehemu mbalimbali, hivyo ni jukumu la serikali kuchukua hatua za kuwalinda wanafunzi dhidi ya mambo hayo. Sambamba na kufunga kamera hizo, Mtaka aliwakumbusha walimu juu ya wajibu wao kubeba dhamana ya wazazi na walezi kwa wanafunzi hao ikiwamo kuwalea kwa misingi inayotakiwa na kuwakinga dhidi ya vitendo vya unyanyasaji.

Ni hakika kwamba mmomonyoko wa maadili katika taasisi za elimu zikiwamo shule za sekondari umezidi kuwa tatizo kutokana na baadhi ya walimu na watumishi kutuhumiwa kushiriki katika vitendo hivyo viovu. Baadhi ya walimu wamedaiwa kuwalawiti na kuwabaka wanafunzi ambao kiuhalisi ni kama watoto wao wa kuwazaa, jambo ambalo linasababisha kuleta doa kubwa katika elimu.

Licha ya baadhi ya walimu kudaiwa kushiriki matendo hayo, baadhi ya wakuu waliopewa dhamana ya kuongoza taasisi hizo, wamekuwa washiriki katika kuwakandamiza wanafunzi wanaotoa taarifa au hata kuwafukuza shule na kuwapatia adhabu kali kwamba wanawasingizia walimu wao.


Wazo lililotolewa na RC Mtaka limekuja kwa wakati mwafaka, hivyo jitihada za makusudi zifanyike ili kamera hizo zifungwe haraka na hatimaye kuwabaini baadhi ya walimu na watumishi wanaoshiriki katika maovu hayo. Ni Dhahiri kwamba wazo la Mtaka itakuwa njia mojawapo ya kukomesha vitendo hivyo vinavyotweza utu na kuvunjia heshima walimu waliopewa dhamana ya kuwalea watoto kwa niaba ya wazazi na walezi.

Ni vyema serikali kupitia Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ikaunga mkono wazo hilo na kuchukua hatua zinazostahili bila kuchelewa. Ni wazi kwamba hata wazazi wakishirikishwa kuchangia ununuzi wa kamera hizo, kwa kuwa wazo lililotolewa ni zuri, watapokea kwa mwitikio chanya na hatimaye kutekeleza azma hiyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Wazazi, tunamlea hivi mwanafunzi, kuanzia shule hadi awapo nyumbani

Na Happy Peter

**ELIMU** ni ujuzi au mafunzo ambayo mtu au watu wanapata kwenye mazingira wanayoishi kama vile ndani ya familia au jamii inayowazunguka.

Zipo elimu za aina mbili; ya kwanza ni elimu rasmi ambayo inatolewa na mtu au watu katika shule na katika nyumba za ibada kupitia viongozi wa dini.

Aina nyingine ni elimu isiyo rasmi ,ambayo mtu hujifunza mwenyewe pasipo kufundishwa, kwa mfano muda wa kula mtoto akiona wazazi wananawa mikono kabla na baada ya kula na yeye atanawa, pia akiona watu wa rika fulani wanasalimiwa na yeye akiwaona ni dhahiri atawasilimia pia .

Elimu ninayozungumzia ni ile ya darasani, ambayo inamuwezesha mtoto kufahamu jinsi ya kuhesabu, kusoma na kuandika (KKK) ambazo ni misingi mama ya taasisi ya elimu.

Hakuna mtu atakayeweza kusoma ikiwa hajui kuandika, wala akaweza kuandika wakati huo huo hajui kusoma, kwa sababu hawezi kujua alichokiandika.

Elimu ya darasani ambayo wanafunzi wanapewa ni sawa, lakini swali ni je, kwanini baadhi ya wanafunzi wa darasa moja wanafanya vizuri wakati wengine wa darasa hilohilo wanafanya vibaya, wakati mwalimu ni mmoja na darasa ni moja pia?

Pia, kuna cha kujiuliza, kwanini ni muhimu mtoto anapofikisha umri wa miaka mitatu apelekwe shuleni? Jibu ni wazi, kwamba huwa mara baada ya kuzaliwa, ubongo wake mtoto huwa mithili ya karatasi nyeupe isiyo na maandishi yoyote ndani.

Kwa hiyo, ni rahisi ubongo huo kuhifadhi chochote kiwe kizuri au kibaya. Hivyo basi, kila anachoona, kusikia na kushika ndicho kinachoanza kujiandika na kujihifadhi ndani ya kichwa au katika ubongo wake.

Hapo ndipo wazazi au walezi wanatakiwa kuwa makini na yale wanayofanya na kuongea wakiwa na watoto wao.

Siku hizi sio ajabu kumsikia mtoto anaongea lugha za matusi, wengine wanavuta bangi, wengine wanawatendea mabaya yasiyosemeka, kinyume na hali zote za ubinadamu.

Vilevile, wapo wenye heshima na busara, wacha Mungu na wanye hofu ya Mungu! Haya yote ni kutokana na mazingira yanayo wazunguka.

Mtoto akiwa katika umri huo, ni dhahiri kwamba ubongo wake unakuwa na kiwango na nafasi kubwa ya kuelewa, hata akaweka mambo kichwani, kitu kinachompa uwezo mkubwa wa kufanya vizuri darasani na kwenye jamii.

Hilo linafahamika kwamba, shuleni siyo elimu za masomo tu, bali hata namna ya kuishi na jamii. Mtoto aliyeanza masomo akiwa na umri mdogo, kamwe huwezi kumfananisha na ambaye ameanza masomo akiwa na umri mkubwa, mfano miaka sita na kuendelea.

Kitaaluma hawawezi kuwa sawa na jamii ifahamu kwenye jambo la taaluma, hakuna ushirikina, ni wajibu watoto wapelekwe mapema.

Kwa upande wa maadili, ni mara chache kuona mtoto anayesoma akaongea kauli za matusi, hasalimii waliomzidi umri, hasaidii wazazi kazi, lakini kwa watoto ambao hawapo shuleni, hilo jambo linawanyemelea na katika baadhi ya jamii, ni la kawaida, hata wakionywa bado wanarudia yale yale.

Elimu wanayotakiwa kupatiwa watoto siyo ile ya darasani peke yake, bali wanapatiwa mila, utamaduni na desturi.

Elimu hii itasaidia kupunguza mmonyonyoko wa maadili ikiwamo kujiingiza kwenye matendo yasiyofaa ndani ya jamii inayomzunguka, kama uvutaji wa bangi na utumiaji dawa za kulevya na lugha za matusi.

Katika suala la umuhimu wa elimu sio tu walimu ndiyo wanatakiwa kuwa kipaumbele, la hasha wazazi na walezi nao wanapaswa kufuatilia maendeleo ya watoto wao wanapotoka shuleni, ikiwamo kuwauliza au kudadisi walichosoma siku husika.

Pia, ni wajibu wao kutoa adhabu pale inapobidi kutokana na makosa wanayofanya, ikiwa ni pamoja na kutoandika wanachofundishwa darasani. Hiyo itasaidia kumjenga mtoto kuzingatia masomo na mafundisho mengine atakayopewa kulingana na umri wake.

Ni jukumu la kila mzazi au mlezi kuhakikisha mtoto anakuwa kwenye mazingira rafiki, ikiwa ni pamoja na kuwapeleka shule kwa wale wanaostahili kulingana na umri wao.

Kwa bahati sasa, serikali inatoa elimu bure kuanzia darasa la kwanza hadi kidato cha nne, ili kutoa fursa kwa mzazi asiye na uwezo kumpeleka mtoto shuleni.

## HABARI KITAIFA

# TIRA yasisitiza bima mikopo SACCOS

**Na Romana Mallya**

KAMISHNA wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), Dk. Baghayo Saqware, ameitaka Kampuni ya Teknolojia ya Mfumo wa Huduma za Kifedha ya Wakandi Tanzania pamoja na wanaosimamia vyama vya ushirika vya kuweka na kukopa (SACCOS) kuhakikisha mikopo yote inayotolewa inakuwa na bima ili kuokoa wateja na vyama.

Ametaka wajikite kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa bima ya maisha na nyingine ili kujikinga na majanga mbalimbali ya kiuchumi na kijamii.

Dk. Saqware aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa bidhaa mpya ya bima ya ulinzi wa mikopo ya Wakandi Tanzania inayotolewa kwa kushirikiana na kampuni ya Sanlam.

Aliwataka pamoja na kutoa huduma, watoe elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa bima ili kuongeza uelewa mpana na kuongeza kasi ya watumiaji.

Kamishna huyo alisema matumaini yake ni kuwa itasaidia kuboresha usalama wa fedha na wanachama wa Saccos na kuongeza mchango wa ukuaji wa sekta ya bima.

"Ushauri wangu kwa Wakandi, SACCOS na wakala unaosimamia vyama vya ushirika ni vizuri kuhakikisha kwamba, mikopo yote ya wanachama hailengi vyama vya ushirika kupata hasara pindi mwanachama anaposhindwa kulipa," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Wakandi Tanzania, Daud Boaz, alisema kampuni yake inajihusisha zaidi na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwa taasisi za kifedha na vyama vya ushirika hasa katika eneo la akiba na mikopo.

Alisema wamekuwa wakitoa huduma ya mifumo kuvisaidia vyama vya ushirika kupata mfumo wa utendaji wao.

"Bado vyama vingi vinafanya shughuli zao kwa kutumia makaratasi na kalamu. Tunachokifanya ni kuviwezesha kuvipa mfumo utakaorahisisha shughuli zao za kila siku. Faida kubwa ni kufanya kazi zao saa 24 na upatikanaji wa ripoti na utunzaji wa taarifa unakuwa wa kisasa zaidi kupitia simu au kompyuta.

"Leo (juzi) tumejizatiti zaidi kutoa huduma moja ambayo vyama vingi vimekuwa vikiikosa ambayo ni huduma ya bima kidigitali tunashirikiana na Sanlam. Ikiwa mwanachama ameomba mkopo unatoka ukiwa na bima," alisema.

Alisema utaratibu wa zamani kwamba mwanachama wa ushirika akifariki dunia familia ndiyo inasumbuliwa, kupitia mfumo huo sasa, Sanlam itabeba deni husika pamoja na gharama za mazishi.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Sanlam, Julius Magabe, alisema lengo la kuanzisha bidhaa hiyo mpya ya bima ni kuboresha usalama wa kifedha na ustawi wa vyama vya ushirika wa akiba na mikopo kwa kuwapa fursa ya kujikinga na hatari za kifedha.



Mkuu wa wilaya ya Nachingwea, mkoani Lindi, Mohamed Moyo (wa pili kushoto), akizungumza na maofisa wa wanyamapori wakati wa zoezi la kuwaondoa tembo kwenye makazi ya watu na kuwarudisha hifadhini katika kijiji cha Narungombe juzi. Wengine ni Mtafiti Mkuu TAWIRI, Dk. Emmanuel Masenga (kulia), Katibu wa mbunge, George Martin (wa pili kulia) na Kamanda wa Uhifadhi Kanda ya Kusini Mashariki wa TAWA, Abraham Jullu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC aonya NGO mmomonyoko maadili

**Na Mashaka Mgeta,** TANGA

MASHIRIKA Yasiyo ya Kiserikali (NGO) mkoani Tanga, yameonywa kutotumika kama sehemu ya kumomonyoa maadili na kushiriki mipango inayochochea utakatishaji wa fedha haramu.

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Waziri Kindamba, alitoa onyo hilo wakati akifungua Mkutano wa Mwaka wa Jukwaa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGO) wenye kaulimbiu 'Mashirika Yetu, Maadili Yetu, Tanga Yetu', uliohitimishwa jana jijini hapa.

Kindamba alisema hivi sasa, jamii imeathirika kwa kiwango kikubwa kutokana na kukithiri kwa mmomonyoko wa maadili unaohusisha vitendo viovu kama vile ushoga, ulawiti na usagaji.

"Tunapitia changamoto kubwa ya mmomonyoko wa maadili kwenye jamii yetu. Ziko NGO zinazotajwa kujihusisha na vitendo hivyo ambavyo kimsingi ni mambo ambayo hata ibilisi hakuyafanya," alisema.

Pia Kindamba alizitaka NGO mkoani Tanga kutotumika kama 'mirija' ya kutakatisha fedha haramu zinazopatikana kutoka kwenye mitandao ikiwemo inayohusika na ugaidi na biashara haramu za usafirishaji binadamu na dawa za kulevya.

Aliziasa NGO kuwa na mipango yenye kuimarika katika nyanja za fedha na wataalamu, badala ya kuwa tegemezi kwa wafadhili wakiwemo wanaowalazimisha kujihusisha na vitendo vinavyokiuka maadili kama masharti ya kupata misaada.

'Wakati wa uongozi wangu hapa Tanga, tutakuwa wakali sana.

Hatutakuwa na tabasamu dhidi ya vitendo vya mmomonyoko wa maadili na biashara haramu za kutakatisha fedha, kusafirisha binadamu na dawa za kulevya, alionya.'

Mwenyekiti wa Bodi ya Uratibu wa NGO nchini, Mwantumu Mahiza, alisema taasisi hizo zinapaswa kufuata sheria, kanuni na taratibu ili kujiimarisha zaidi na kuepuka kufutiwa usajili.

Alisema ufuatiliaji shughuli na uendeshaji wa NGO unafanywa kwa njia ya mfumo, hivyo kuondoa dhana kwamba inafanywa na mtu binafsi.

Alizitaka NGO kutekeleza majukumu yao ipasavyo ili kufikia lengo la kuisaidia serikali katika kupata suluhu ya kero zilizopo kwenye jamii.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Tanga, Pili Mnyema, aliziagiza NGO mkoani hapa kuwasilisha taarifa zao serikalini ili kufanikisha azma ya utaratibu na usimamizi wa shughuli zao, kwa mujibu wa sheria.

"Hatuwezi kuwasimamia na kuwaratibu kama hatuwafahamu. Bila sisi kuwajua, itakuwa vigumu kutoa huduma mnapohitaji. Hivyo timizeni wajibu wa kisheria kuwasilisha taarifa zenu kwa ukweli na uwazi", alisema.

## KABWELA

Na Fadhili Mohammed



# Waziri atahadharisha wanaotumia wizara kufanya matukio ya uhalifu

**Na Munir Shemweta**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amewatahadharisha watu wanaotumia wizara yake kama rejea kufanya uhalifu na kujipatia mali au fedha isivyo halali.

Dk. Mabula amesema mtu yeyote akihisi kuna udanganyifu ndani na nje ya wizara, atoe taarifa mapema ili kukomesha uhalifu huo.

Mabula alisema hayo juzi jijini hapa kutokana na wizara yake kupokea malalamiko ya muda mrefu kutoka kwa familia ya marehemu Zuberi Mwinyimvua inayodai kwamba wizara yake haitaki kuondoa hati ya kuwekeza iliyosajiliwa katika daftari la Msajili wa Hati kuhusu kiwanja Na 895 kilichoko eneo la viwanda Mbezi, Dar es Salaam iliyosajiliwa ili kutoa kinga ya uwekezaji.

Kwa mujibu wa Dk. Mabula, kiwanja hicho kinamilikiwa na Mwinyimvua ambaye kwa sasa ni marehemu.

Alisema awali mmiliki wa kiwanja hicho aliingia mkataba wa uwekezaji na Velence Simon Matunda na Badi Nkya wanaotambulika kama wawekezaji.

Uwekezaji huo ulikuwa kujenga maduka 40 na kati ya hayo maduka 33 yangesimamiwa na wawekezaji kwa kipindi cha miaka 15 na baada ya hapo wangekabidhi maduka 15 kwa mmiliki na katika kipindi hicho cha miaka 15 wawekezaji wangekusanya kodi ya pango.

Kwa mujibu wa mkataba, mmiliki alipewa Sh. 90,000,000 kwa ajili ya kulipa madeni ikiwamo kodi ya pango la ardhi la kiwanja hicho. Waziri Mabula alisema mgogoro huo umekuwa ukishughulikiwa kiutawala kupitia wizara kwa takribani miaka minane kuhakikisha wawekezaji wanalipwa fedha hizo kama mahakama ilivyoamuru ili hatimaye msajili wa hati aondoe hati ya kuwekesha katika daftari la msajili na kukabidhi hati husika.

Kwa mujibu wa Waziri Mabula, mpaka sasa suluhu ya mgogoro huo haijapatiakana kutokana na pande mbili za mgogoro, yaani msimamizi wa mirathi na wawekezaji kutotekeleza yale waliyokubaliana hususan upande wa uwekezaji.

Kimsingi, mgogoro huo unatokana na ukiukwaji wa makubaliano baina ya mmiliki na wawekezaji ambapo pia mahakama ilishatoa uamuzi. Wizara inatimiza wajibu wake kiutawala katika kutatua mgogoro pamoja na kuwa suala hilo linahusu mkataba wa uwekezaji na si umiliki wa ardhi.

Waziri Mabula alisema kwa kuwa mgogorio huo ni wa muda mrefu na wahusika wanaihusisha wizara ambayo si sehemu ya makubaliano, hivyo kuharibu taswira ya wizara, ameelekeza pande zote za mgogoro kuheshimu na kutekeleza hukumu ya mahakama sambamba na pande hizo kutekeleza yale wanayokubaliana katika vikao vya usuluhushi.

Pia alimwelekeza katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kushirikiana na vyombo vya dola kuingilia kati suala hilo kwa kuwa lina sura ya kijinai na utapeli ndani yake.




Meneja Mradi wa Kampuni ya Superbrands, Jawad Jaffer (wa pili kulia), akiwakabidhi tuzo Watendaji wa Shirika la Bima ya Taifa (NIC), wakati wa utoaji wa tuzo za Superbrands kwa kampuni zinazofanya vizuri katika kutoa huduma vizuri kwa wateja, jijini Dar es Salaam juzi. Katikati ni Mkurugenzi Mtendaji wa shirika hilo, Dk. Elirehema Doriya. **PICHA NA JUMANNE JUMA**

# Aliyejeruhiwa na fisi afariki dunia

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

MKAZI wa kijiji cha Chiwambo, Kata ya Lulindi, Masasi mkoani Mtwara, Rashid Yusuph (60) ambaye alijeruhiwa na fisi miezi miwili iliyopita amefariki dunia. Yusuph alifariki dunia juzi katika Hospitali ya Mission Ndanda wilayani Masasi alikokuwa akipatiwa matibabu baada ya kukutwa na masahibu hayo mwishoni mwa mei, mwaka huu baada ya fisi huyo kujeruhi watu wawili na kuua mmoja kijijini hapo.

Akizungumza na mwandishi wa Habari hii kwa njia ya simu akiwa katika hospitali hiyo, mtoto wa marehemu, Hamisi Rashidi, alisema baba yake amefariki dunia juzi baada ya kuugua kwa muda mrefu majeraha aliyekuwa ameyapata baada ya kuvamiwa na mnyama huyo.

Rashidi alisema baba yake tangu alipopata majeraha hayo, hali yake ya kiafya imekuwa mbaya na kwamba alikuwa akiugulia nyumbani kwa kupata dawa za kutuliza maimivu.

Alisema alipata majeraha sehemu mbalimbali za mwili wake hasa maeneo ya kichwani, usoni na tumboni hali ambayo ilionekana majareha hayo kutopona hadi ikusababisha kupoteza maisha. Kutokana nah al;I yake kuwa mbaya, walichukua uamuzi wa kumpeleka hospitali ya Misison Ndanda na alipokewa na kulazwa hadi juzi saa 11:00 jioni alipofariki dunia.

Mtoto wa marehemu alisema tayari wameshachukua mwili kwa ajili ya kuupeleka kijijini Chiwambo ili kuendelea na taratibu za maziko.

Baadhi ya wananchi wa kijiji hicho waliozungumza na gazeti hili jana mara baada ya taarifa za majeruhi huyo kufariki dunia, walisema wamepokea kwa masikitiko taarifa za kifo hicho.

Kutokana na tukio hilo, wamesema watahakiisha wanapambana na fisi walioko katika kijiji chao ili kukomesha matukio ya wananchi kuuawa na kujerahiwa na wanayma hao ambao wamekuwa wakivamia wananchi na kufanya uhalifu.

Hassani Bakari, mkazi wa kijiji hicho alisema wanaiomba serikali kuwaondoa fisi katika eneo hilo kwa sababu matukio ya wanyama hao kujeruhi wananchi ni mengi

Naye Fatuma Saidi mkazi wa kijiji cha Chiwambo alisema kwa sasa wananchi wamekuwa wakiingia ndani ya nyumba zao kuanzia saa 12 jioni kwa kuhofia wanyama hao wakali kwa kuwa ikifika majra hayo kumekuwa na makundi mengi ya fisi wakizunguka kwenye maeneo yao hali ambayo imekuwa ikijenga hofu dhidi ya maisha yao.

# PPRA yasisitiza usajili wa NeST

**Na Frank Monyo**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) imewasisitiza wafanyabiashara na wazabuni wote nchini kuendelea kujisajili katika mfumo mpya wa ununuzi wa umma kwa njia ya mtandao (NeST) ili kuongeza ushindani na kupanua wigo mpana katika kuboresha uendeshaji wa michakato ya ugawaji wa zabuni za umma.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa PPRA, Eliakim Maswi, alisema janakuwa idadi ya wazabuni wanaojisajili kwenye mfumo inazidi kuongezeka siku hadi siku jambo linalotoa taswira chanya juu ya muitikio na mapokeo ya wananchi katika ujio wa Mfumo huo mpya.

"Tunashkuru kupitia juhudi za serikali yetu kuona idadi ya wazabuni wanaojisajili ndani ya mfumo inaongezeka siku hadi siku suala ambalo hata sisi kama mamlaka tunalitazama kwenye mtazamo Chanya. Mpaka sasa wazabuni 4,350 tayari wameshajisajili kwenye mfumo," alisema Maswi.

Sambamba na suala hilo, Maswi aliwataka Wazabuni pamoja na Taasisi za Umma kuendelea kushiriki mafunzo yanayoendelea kutolewa katika mikoa mbalimbali nchini ambayo yanalenga kutoa muongozo wa namna ya matumizi sahihi ya Mfumo huo wa NeST kwa Taasisi za Umma sambamba na Wazabuni wake.

"Utaratibu wetu wa utoaji mafunzo ya jinsi ya kutumia mfumo bado unaendelea. Kwa hiyo niwasihi wazabuni na taasisi mbalimbali za umma kushiriki mafunzo hayo kwa mujibu wa ratiba zinazopangwa" alisisitiza.

Sambamba na utoaji wa mafunzo hayo wanahakikisha kila taasisi inayopatiwa mafunzo inasajiliwa ndani ya mfumo wa NeST ili kuanza mapema kutumia mfumo huo bila kuwa na urasimu wa aina yoyote.

"Kila taasisi tunayoipatia mafunzo ya mfumo mpya tunahakikisha tunaisajili pia kwenye mfumo ili ikibidi waanze kutumia mfumo huu haraka," alisema.

Ifikapo Septemba 30, mwaka huu, taasisi zote za umma zinatakiwa ziwe tayari zimeshajisajili kwenye mfumo kwa kuwa mpaka Oktoba Mosi, mwaka huu, hakutakuwa na taasisi yoyote ya umma itakayofanya michakato ya ununuzi nje ya NeST.



## Kampeni uhamasishaji matumizi nishati safi yazinduliwa

**Na Mwandishi Wetu,**
ARUSHA

KAMPENI ya kuhamasisha matumizi ya nishati safi imezinduliwa ikiwa na lengo la kuunga mkono jitihada za serikali kwenye matumizi nishati salama kimazingira.

Akizungumza wakati uzinduzi wa kampeni hiyo jijini hapa, Mkurugenzi wa Kampuni ya Sola D. Light Tanzania Ltd, Charles Natai alisema lengo kubwa la kampeni hiyo ni kuhamasisha Watanzania kutumia nishati safi ya sola ili kuleta mapinduzi ya matumizi ya nishati ya jua nchini badala ya nishati zinazohatarisha mazingira na tabaka la ozoni.

"Kampeni hii inalenga kuwapa hamasa wateja kuhamia kwenye nishati safi na sisi kama D. Light tumeona ni vyema kutambua mchango wa kila mteja wa kweli.

"Hivyo basi, tunapenda kuwataarifu kuwa tutakuwa tunawazadia kila mwisho wa mwezi, hii ni kwa wateja wetu wa sasa ambao bado hawajarudisha mikopo yao au kulipa kwa wakati, lakini pia kwa wateja wapya watakaojiunga nasi," alisema.

Mmoja wa mawakala wa kampuni hiyo, Madinda Juma alisema tangu ameanza kunua bidhaa imemsaidia kukua kimaisha, kukuza kipato pamoja na kujenga nyumba.

Kampuni hiyo tayari imewasadia watu zaidi ya milioni 100 Afrika na watu wapatao 200,000 Tanzania katika matumizi ya nishati safi ya sola.

Kampeni hiyo inajulikana kama 'Mwanga wako, mchongo wako' itawapatia fursa wateja wenye bahati kujishindia zawadi mbalimbali kama vile mfumo wa nishati ya jua kwa matumizi ya nyumbani watakapolipa siku 90 kwa mkupuo, baiskeli, simu janja na vifurushi vya muda wa maongezi vya Sh.20,000 wakimaliza malimbikizo ya mikopo yao.

## Madiwani wakunwa utekelezaji miradi ya maendeleo

**Na Allan Isack,**
ARUMERU

MADIWANI katika Halmashauri ya Arusha wamewapongeza watalamu wa halmashauri hiyo kwa utekelezaji wa shughuli za miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Licha ya kutoa pongezi hizo wameishukuru serikali kwa kuwapatia fedha nyingi za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwenye halmashauri hiyo.

Walitoa pongezi hizo jana baada ya Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Seleman Msumi, akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa shughuli za maendeleo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 wakati wa mkutano maalum wa baraza la madiwani wa mwaka.

Mkurugenzi huyo alisema kuwa halmashauri imefanikiwa kukusanya mapato ya Sh.bilioni 4.8 kutoka bajeti ya Sh.bilioni 4.8 sawa na asilimia 101.24.

Aidha, alisema kwa mwaka huo halmashauri hiyo imetekeleza miradi ya maendeleo baada ya kuidhinishiwa na Bunge Sh.bilioni 11.8 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Msumi alisema walipokea Shilingi bilioni moja fedha za nje ya bajeti na kutumia Sh.milioni 980 sawa na asilimia 89.8, huku kukiwa na bakaa ya Sh.milioni 53 kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Ojung'u Salekwa, aliipongeza halmashauri na kuishukuru serikali kwa kutoa fedha nyingi zilizotekeleza miradi ya maendeleo.

Diwani wa Kata ya Oljoro, Sanare Mepalary, alisema licha kupongeza utekelezaji wa shughuli hizo pia alithibitisha kuvutiwa na hali ya kuimarika kwa ukusanyaji wa mapato hasa kwenye chanzo cha mchanga Mirongoine, akisema hali hiyo imefanikisha kuongeza mapato na kuvuka malengo.

# Ndumbaro: Katiba mpya siyo mali ya wanasiasa

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Dk.Damas Ndumbaro amesema suala la katiba mpya sio mali ya wanasiasa bali ni mali ya kila mtu, hivyo ni muhimu kuwashirikisha wananchi kwenye kila hatua. Aliyasema hayo jana jijini Arusha wakati wa uzinduzi wa Bodi ya Kitaifa ya Ushauri wa Msaada wa Kisheria.

Alisema katiba siyo ya wanasiasa bali ni ya wananchi wote, hivyo lazima wananchi washirikishwe kutoa maoni yao ili pale mahali palipokosewa parekebishwe.

Aidha, aliiomba bodi hiyo ya msaada wa kisheria iwashauri zaidi katika kupata katiba mpya ijayo, itakayodumu kwa zaidi ya miaka mingi kwani Watanzania hivi sasa wanataka katiba mpya.

Pia aliagiza bodi hiyo ikutane kama inavyotakiwa ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma muhimu za msaada wa kisheria, katika utatuzi wa mambo mbalimbali ya kisheria nchini.

Aidha, aliitaka bodi kuhakikisha wanajengeana uwezo na viongozi mbalimbali, uwepo wa shughuli mbalimbali za ushauri wa msaada wa kisheria ili kuhakikisha wananchi wanaelewa majukumu ya bodi hiyo na usawa mbele ya sheria.

Kadhalika, alisema nchi chache za Afrika ndiyo zina bodi za msaada wa kisheria, hivyo alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuhakikisha haki za binadamu na wanyonge zinapatikana na kutatuliwa kwa haraka.

Alisema jukumu la bodi ni kuangalia jinsi ya kushirikiana na watoa huduma za msaada wa kisheria, wanafanyaje kazi kuanzia ngazi za kata, shina, wilaya na mikoa.

Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria, Mary Makondo aliishukuru serikali, kwa kuhakikisha wanawake, wanaume, watoto, watu wasio na uwezo, wazee kupata msaada wa kisheria bure nchini.

Naye Mjumbe wa bodi hiyo, Faraja Nchimbi, kutoka Ofisi ya Taifa ya Mshataka, alisema bodi hiyo inamshauri Waziri wa Katiba na Sheria juu ya haki kutendeka.

Alisema bodi hiyo na menejimenti wamejifunza mada mbalimbali za kisheria ikiwemo masuala ya fedha zinazoratibu huduma za msaada wa kisheria.



Mkurugenzi Mkuu wa D.light Tanzania, Charles Natai, akizindua zawadi ya kampeni yao iitwayo "Mwanga Wako, Mchongo Wako", jijini Arusha juzi, inayolenga kuhamasisha watu kwenye matumizi ya nishati safi ya jua nchini ambapo wananchi watajishindia zawadi mbalimbali kwa kipindi cha miezi miwili. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

## Shule za msingi, sekondari zapokea msaada madawati, vifaa

**Na Mary Mosha,** SAME

SHULE za msingi na sekondari katika Kata ya Kirangare wilayani Same mkoani Kilimanjaro, zimepata msaada wa madawati na vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya kuwasaidia katika elimu.

Msaada huyo ni pamoja na madawati 300 kwa ajili ya shule za msingi, projekta, kompyuta mpakato, mashine ya kurudufu kwa shule za sekondari.


Akizungumza wakati wa kukabidhi msaada huo ,Mbunge wa Same, Anne Kilango, alisema alilazimika kutafuta msaada huo baada ya kufika Shule ya Msingi Parane na wanafunzi walimlilia kutokana na uhaba wa madawati.

Baadhi ya walimu waliopokea msaada huo, akiwemo Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Kirangare, Simon Mweta, alisema wamepokea kompyuta mpakato tano, monita tano na UPS tano, printa moja na projekta moja.

Alisema msaada huo utawasaidia wanafunzi kupata elimu kuhusu mada zitakazofundishwa na walimu wataweza kufundisha na kumaliza mada kwa wakati.

Mkuu wa Shule ya Msingi Parane, Mariselino Bee alisema upatikanaji wa madawati hayo unaenda kupunguza upungufu wa madawati kwa asilimia zaidi ya 80 kwenye shule hiyo.

Mkurugenzi wa Halmashauri Same, Anastasia Tutuba, alisema madawati yaliyokuwapo mengi yanahitaji ukarabati kwa kuwa kila mwaka wanatenga fedha pamoja na kuwashirikisha wadau mbalimbali hapa nchini.





# Ukosefu vyoo bora chanzo wanafunzi kujisaidia vichakani

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

WANAFUNZI wa Shule ya Msingi Kiloleli wilayani Kishapu mkoani Shinyanga wanajisaidia vichakani baada ya vyoo katika shule hiyo kujaa.

Kero hiyo iliibuliwa juzi na Mwalimu Mkuu Msaidizi katika shule hiyo, Juliana Petro, na kueleza kuwa shule hiyo ina wanafunzi 997 lakini kwa sasa wanakabiliwa na tatizo la ukosefu wa vyoo.

Alisema vyoo vilivyokuwapo ni vibovu havifai tena kwa matumizi na wanafunzi wamekuwa wanajisaidia vichakani.

Aidha, alikishukuru Kituo cha Taarifa na Maarifa kutoka Kata ya Kiloleli, ambacho kimekuwa kikijengewa uwezo na Mtandao wa Jinsia Tanzania(TGNP) kuibua kero hiyo kisha kuanza kuitafutia ufumbuzi kwa kushirikiana na wananchi.

Mjumbe wa kituo hicho, Helena Makelele, alisema baada ya kuibua kero hiyo ndipo wakaona washirikiane na uongozi wa kijiji, kisha kuitishwa mkutano wa hadhara na wananchi kuhamasika na kuanza kujenga matundu 24 ya choo.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kiloleli, Kuhwema Mshala, alisema katika mkutano huo wanakijiji walikubaliana kuchangia Sh. 2,000 kwa kila kaya pamoja na kujitolea kuchimba shimo la choo, huku kituo hicho wakitoa Sh.50,000 na mifuko mitano ya saruji.

Alisema mbali na michango hiyo ya wananchi pia katika kikao cha kata walichangia mifuko 30 ya saruji, serikali ya kijiji nayo ilitoa Sh.600,000, Jeshi la Jadi Sungusungu walitoa Sh.500,000 na kisha kuanza ujenzi na sasa wapo hatua ya lenta.

Mtendaji wa kijiji hicho, Nicholaus Mzirai, alisema katika fedha walizopata kutoka katika ushuru wa pamba Sh. milioni 1.3, walikubaliana itolewe Sh. 500,000 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa matundu hayo kunusuru afya za wanafunzi.

## Wenye ulemavu waomba msaada vifaa vya kutembelea

**Na Shaban Njia,** KAHAMA.

WATU wenye ulemavu katika Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga wamewaangukia wadau na serikali kuwasaidia vifaa vya kutembelea ili wafanye kazi na kujiingizia kipato.

Haya waliyabainishwa jana Kata ya Uyogo wakati kampuni ya kununua tumbaku iitwayo JTI ilipokuwa ikitoa msaada wa madawati 350, sare za shule kwa wanafunzi 170.

Pia walitoa msaada wa baiskeli za magurudumu matatu 6, fimbo nyeupe 50 kwa watu wenye uoni hafifu na fimbo za kutembelea ikiwa na thamani ya Sh. milioni 57.5.

Mkazi wa Uyogo, Charles Mabula ni miongozi mwa watu walemavu waliopewa baiskeli za magurudumu matatu alisema, kukosa vifaa vya kuwawezesha kutembea kunawasababishia kushindwa kujishughulisha na biashara.

Alisema kwa msaada waliopewa utawezesha kushiriki shughuli mbalimbali za kijamii ikiwemo kilimo tofauti na ilivyokuwa awali.

Hivyo waliwaomba wadau wa maendeleo kwa kushirikiana na serikali kuendelea kuwawezesha vifaa mbalimbali ili waondokane na umaskini kwani wengi wametelekezwa na watoto wao katika mahitaji.

Naye Juma Shabani, mwenye uoni hafifu alisema, ana nguvu ya kuweza kufanya kazi lakini kulingana na tatizo alilokuwa nalo anashindwa kujihusisha na jamii na kufanyakazi.

alisema kwa msaada wa fimbo aliyopewa atahakikisha anazalisha zaidi mazao ya chakula na biashara na kujiingizia kipato cha kaya.

Awali akikabidhi vifaa hivyo katika Ofisi ya Mbunge wa Ushetu, Meneja Miradi wa JTI, Oscar Lwoga alisema msaada walioutoa kwa vyama vya msingi vitano walivyoingia navyo mikataba ya uzalishaji wa tumbaku.

Alivitaja kuwa ni Mliza, Mshikamano, Mwanzugi, Imaleaseko na Mwadui.

Mrajisi Msaidizi wa vyama vya ushirika mkoani shinyanga, Hilda Boniphace, aliipongeza kampuni hiyo kwa kutoa vifaa ambavyo vitawezesha kuinua elimu na kutatua changamoto zinazowakabili watu wenye ulemavu.

Hivyo alizitaka kampuni zingine husùsani zinazonunua zao la pamba kuiga mfano huo kurejesha sehemu ya faida katika jamii.

Naye Ofisa Tarafa, Tarafa ya Dakama, Tumshukuru Mdui alisema, madawati hayo yatakwenda kutumiwa na wanafunzi 1,050 kwa wastani wa madawati 45 kila darasa na kila mmoja kutumiwa na wanafunzi watatu.

Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Cherehani, alisema kampuni hiyo imekuwa mstari wa mbele katika kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili wananchi na hivi karibu walichimba visima vya maji safi na salama na kukabidhi zahanati ya kisasa katika Kata ya Ubagwe ikiwa na thamani ya Sh. milioni 290.

Alisema kuwa zahanati hiyo imesaidia wananchi hasa wajawazito kutotembea umbali mrefu kutafuta huduma za uzazi na kutozwa faini ya Sh.50,000 kwa wale walikuwa wakijifungulia nyumbani au kwa waganga wa jadi.

Alisema kwa sasa JTI inatoa madawati, sare za wanafunzi na vifaa kwa wenye ulemavu.




Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Kilimanjaro, Patrick Boisafi (wa pili kushoto), akikabidhi dawati moja, kompyuta na printa kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same, Anastasia Tutuba, ikiwa sehemu ya vifaa vyote vilivyokabidhiwa katika Shule ya Sekondari ya Kata ya Kirangare, wilayani humo juzi, vilivyotolewa na Mbunge wa Same Mashariki, Anne Malecela. **PICHA: MARY MOSHA**

## Jamii yakumbushwa kujikinga dhidi ya UKIMWI

**Na Timothy Itembe,** MARA

JAMII imetakiwa kuchukua hatua za kujikinga na Virusi Vya Ukimwi (VVU) kwa kuzingatia ushauri unaotolewa na wataalamu, lengo likiwa ni kupunguza maambukizi.

Rai hiyo imetolewa juzi na Dk. Florence Temu kutoka (Amref) wakati wa uzinduzi wa mradi wa afya kamilifu unaoshirikisha Mikoa ya Mara, Simiyu na Tanga.

Alisema kuwa jukumu la kupambana na UKIMWI ni la kila mmoja kujilinda mwenyewe.

Dk. Temu alisema kuwa kuna haja jamii kuendelea kuzingatia elimu inayotolewa na wataalamu wa afya juu ya kujikinga na maambukizi mpya ya UKIMWI ikiwa ni pamoja na kuzingatia matumizi sahihi ya kinga na kuwa waaminifu.

"Licha ya kutoa elimu kwa jamii lakini baadhi ya watu wanaendelea kuishi maisha ya mazoea kwa kufanya ngono zembe wakati mwingine kutokutumia kinga na kujihatarisha," alisema.

Kaimu Katibu Tawala Mkoa Mara, Dominicus Lusasi, aliyataka mashirika kuendelea kuweka mkazo katika kujikinga kwa kushirikiana na mashirika binafsi yanayotoa elimu juu ya tatizo hilo.

Naye Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Mji wa Tarime, Elias Makima, alisema mfumo ulioletewa na shirika hilo ni mzuri na matumizi ya mfumo wa utambuzi wa kutumia vidole badala ya makaratasi utasaidia kuwatambua wagonjwa wa UKIMWI na kutunza taarifa kwa siri tofauti na ilivyozoeleka miaka ya nyuma.

Pia, alibainisha kuwa maeneo yanayoathirika zaidi ya maambukizi ni pamoja na Tarime kwa sababu kuna mwingiliano wa watu.

ama
ALHAMISI AGOSTI 17, 2023
AFYA NA MAZINGIRA


Ukurasa 14

## Wachimba madini kinamama wanaowezesha kuwapo zahanati inayowatibu kijijini kwao


Ukurasa 12

## Kinamama wakumbushwa hatari kwa anyonyeshae akisinzia na mtoto wake


Ukurasa 13

## Simulizi ya watoto njiti na maisha wanayoishi

AFYA

# Miaka 15 ya Mpango Afya ya Msingi, makubwa zamu ya Rais Dk. Samia



Jengo la Huduma ya Mama na Mtoto, wilayani Makete, lililozinduliwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI ana miaka mitatu madarakani, ndipo Rais Dk. Jakaya Kikwete, alipozindua Mpango wa Afya ya Msingi (MMAM), leo hii miaka 15 baadaye, si jambo geni, lililoko katika utekelezaji na maboresho katika sura tofauti.

Waliomrithi uongozi, marais wa awamu ya tano Dk, John Magufuli kaidumisha na sasa, Dk. Samia Suluhu Hassan, aliyemsaidia Dk. Magufuli, zamu yake anaiendeleza kwa makubwa kulingana na mahitaji ya matumizi na maendeleo waliyonayo.

Kwa ujumla wake, hatua kubwa zimepigwa, zahanati na vituo vya afya vinatapakaa nchini, halikadhalika hospitali zote za rufani ngazi ya mikoa, zikifika ambako hazikuwapo na kwenye mikoa mipya kama vile Katavi.

Hapo katika zama za Rais Dk. Samia, ikimtoka kinywani kwa mtaalamu wa udaktari na kutumia uwaziri katika Wizara ya Afya, katika nafasi yake ya sasa, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI, Dk. Faustine Ndugulile.

Hafichi hisia za kamati yao, kwamba wanampongeza Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kutumia fedha walizopewa kwa ajili ya kukabili maradhi ya UVIKO, kuboresha sekta ya afya nchini, ili wananchi kupata huduma bora.

Ni kauli ya Dk. Faustine Ndugulile, Hospitali ya Taifa ya Magonjwa ya Afya ya Akili Milembe na Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma, ziko katika ngazi ya hospitali za taifa ya rufani.

Kwa mujibu wa Mpangilio wa MMAM, kiasi cha shilingi bilioni 10 zimetumika kuboresha sekta ya afya katika Hospitali ya Taifa ya Magonjwa ya Afya ya Akili Milembe, ikijumuisha jengo la kisasa na dharura, wagonjwa mahututi na mashine ya mionzi (X-RAY).

Katika Hospitali ya Rufani Mkoa wa Dodoma, nako uwekezaji wa Rais Dk. Samia, umeshuhudiwa na kamati kutembelea jengo la wagonjwa wa dharura na la wagonjwa mahututi, kuona serikali ilivyoboresha maeneo hayo kwa lengo la kutoa huduma bora kwa umma.

Daktari Ndugulile anatoa wito kwa Wizara ya Afya kuongeza nguvu zaidi katika huduma za afya ya akili, akinena matatizo hayo yamekuwa yakiongezeka kwa kasi.

"Ili kuendana na kasi ya kuongezeka matatizo ya afya ya akili nchini, kuna haja ya kusogeza huduma za afya ya akili katika ngazi ya msingi, ili kusaidia wananchi waliopo katika maeneo ya kata, vijiji vyote na katika majimbo yetu," anasema.

**INAENDELEA UK.13**

AFYA

WIKI YA UNYONYAJI IKIAGA...

# Kinamama wakumbushwa hatari kwa anyonyeshae akisinzia na mtoto wake



Mtoa Huduma ya Afya Ngazi ya Jamii, Joyce Temba (kushoto), akimuelekeza Khadija Shabani, jinsi ya kumkalisha mtoto na kumnyonyesha katika kilele cha Wiki ya Unyonyeshaji Kimataifa. **PICHA: SABATO KASIKA**

**Na Sabato Kasika**

PENGINE inaweza kuwa geni ikiwamo kwa baadhi ya kinamama kusikia unyonyeshaji mtoto, nao una utaratibu wake unapaswa kuzingatiwa, ili kuhakikisha wanahali salama.

Utaratibu ambao mzazi hatakiwi kunyonyesha mtoto akiwa amelala, badala yake mtoto anapohitaji kunyonyeshwa wakati wa usiku, mama yake anatakiwa kumchukua na kukaa na kuanza kumnyonyesha.

Hivyo, ndivyo anavyoeleza mtoa huduma ya afya ngazi ya Jamii, Joyce Temba, wakati akitoa elimu hiyo kwa wakazi wa kata ya Kipunguni, Dar es Salaam wiki iliyopita.

Ni katika mkutano wa kuileta jamii pamoja kujadili masuala ya ukatili, kupeana taarifa, maarifa na mirejesho ya hatua zinazochukuliwa kwa yanayoibuliwa, ulioandaliwa na Kituo cha Sauti ya Jamii Kipinguni.

Mada kuu ilikiwa unyonyeshaji, afya ya akili na vyanzo vyake, namna ya kujikinga au kumkinga mwingine na maambukizi ya VVU, ukeketaji na madhara yake.

Mada nyinginezo zilihusu haki za watu wenye ulemavu, hedhi salama, malezi na madhara ya ukatili wa kimtandao na kingono na sehemu sahihi za kutoa taarifa za matukio hayo.

> Wakati ulimwengu ukiadhimisha Wiki ya Kimataifa ya Kunyonyesha mtoto, sisi tumeitumia kutoa elimu ya mambo mbalimbali, kinamama wakifundishwa jinsi ya unyonyeshaji.

Hapo ndipo mtoa huduma huyo wa afya ngazi ya jamii, anajikita zaidi kuelekeza hatari ya mama kunyonyesha mtoto akiwa amelala, kwa kuwa anaweza kumsababishia kifo bila ya kutarajia.

### KIFO KINAVYOTOKEA

Mtaalamu huyo anafafanua kuwa, mama anapomnyonyesha mtoto huku wote wakiwa wamelala, kuna uwezekano wote wakapitiwa na usingizi, ziwa likatoka mdomoni mwa mtoto na kumfunika.

Mtaalamu Joyce anafafanua: "Akifunikwa na ziwa anaweza akakosa hewa na kumsababishia mauti, hivyo, tunashauri iwapo wote wamelala, mtoto akihitaji kunyonya, mama ainuka akae amnyonyeshe, akimaliza ndipo amlaze."

Kwa mujibu wa Joyce, inaweza kuwa jambo geni kwa baadhi ya kina mama, lakini anaongeza kuwa ni vyema wakalizingatia hilo, kwa ajili ya usalama wa watoto wao wanapowanyonyesha.

"Ni muhimu kujua njia sahihi za kunyonyesha, kwani ni rahisi mama kusababisha kifo cha mtoto wake kwa unyonyeshaji vibaya bila kujua na kudhani amechezewa na kumbe ni yeye aliyesababisha," anasema.

### MAZIWA YA MAMA

Joyce anasema, maziwa ya mama yanampatia mtoto virutubisho vyote anavyohitaji, katika miezi sita ya mwanzo tangu azaliwe na kwamba kikwazo ni imani potofu miongoni mwa jamii, kimekuwa kikikwamisha watoto wachanga kupata lishe bora inayostahili.

"Kumekuwa na mtazamo kwamba, maziwa ya kwanza ambayo mama huyapata mara baada ya kujifungua si maziwa kwa mtoto,: anatamka na kufafanua: "Wapo wanawake ambao huyakamua na kuyamwaga hadi yatoke maziwa ya rangi nyeupe, jambo ambalo ni kosa."

Anasema maziwa ya kwanza huwa kama chanjo ya kwanza kabisa kwa mtoto, kwa kuwa yana virutubisho vingi, pia yana kinga zitakazomsaidia mtoto kutopata maradhi mbalimbali siku za usoni.

"Ni vema mtambue kuwa maziwa ya kwanza ya mama ambayo kitaalamu yanaitwa 'colostrum'. Hii colostrum' ndio muhimu zaidi kuliko maziwa yoyote ya mama ambayo atayatoa baadaye," anasema.

Mtoa huduma huyo anasema wataalamu wa afya wamekuwa wakihimiza umuhimu wa watoto wachanga kupata lishe bora ya maziwa ya mama zao, tangu muda mfupi baada ya kuzaliwa.

Anafafanua hayo, huku akielezea muda sahihi wa mtoto kunyonyesha, kwamba ni kuanzia umri anapozaliwa hadi miezi sita pasipo kupewa chakula kingine zaidi ya maziwa ya mama yake.

"Maziwa ya mama asilimia 75 ni maji na asilimia 25 ndio yenyewe (maziwa) ambayo kwa afya ya mtoto ni muhimu katika kipindi hicho na anatakiwa kunyonyeshwa kwa saa 15 (kwa siku)," anasema.

Katika ufafanuzi wake ni kwamba, hata kama mtoto atakuwa amelala mama yake anatakiwa kumuamsha na kumnyonyesha, asisubiri au asichukulie kama njia ya kumwongezea unafuu wa kutombeba.

"Ukiona amelala sana, mwamshe umnyonyeshe, kwani anatakiwa apate ziwa kwa saa zisizopungua 15 kuanzia asubuhi, lakini anapohitaji kunyonyeshwa usiku wakati mmelala, inuka kaa mnyonyeshe," anasema.

Mmoja wa washiriki wa mkutano huo aliyejitambulisha kwa jina la Khadija Shaban, anasema ameongezewa uelewa na kwamba ataupeleka kwa wanawake wenzake, kwa maelezo wengi wao hawana elimu hiyo.

"Binafsi nimezoea kumnyonyesha nikiwa nimelala, kumbe ni hatari, pia ni kawaida kwa wanawake wengi kutowanyonyesha watoto wao kwa miezi sita bila kuwapa kitu chochote," anasema.

Anasema, kuna wanawake wengine wamezoea kuwapa watoto maziwa angali hata hawajafikisha miezi miwili na wapo wanaowapa uji wakiwa na miezi minne, na sasa amegundua ni kosa.

Mkurugenzi wa Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni, Seleman Bishagazi, anasema kila mwezi wana utaratibu wa kuileta jamii pamoja kujadili masuala ya kikatili, kupeana taarifa, maarifa na marejesho ya hatua zilizochukuliwa kwa yaliyoibuka kwenye vikao vilivyopita.

"Wakati ulimwengu ukiadhimisha Wiki ya Kimataifa ya Kunyonyesha mtoto, sisi tumeitumia kutoa elimu ya mambo mbalimbali, kinamama wakifundishwa jinsi ya kunyonyeshaji," anasema Bishagazi, akiwa na ufafanuzi maadhimisho hayo yalifikia kilele chake Agosti 8 mwaka huu.

AFYA

# Simulizi ya watoto njiti, maisha wanayoishi

Na Yasmine Protace

KATIKA tafsiri pana kuhusu kujifungua imekuwa na usemi mtu kajifungua mtoto hajatimia au wengine wanamtaka anayezaliwa 'mtoto njiti.'

Hata hivyo, mada hiyo inapoingia kwa undani, wengi wao hawaelewi vema sababu za kuzaliwa njiti. Wapo wanaofika mbali kwa kuingiza imani potofu pale anapozaliwa mtoto huyo.

Lakini kwao, wataalamu wa uzazi wao wanasema mtoto atazaliwa njiti, anapokuwa hajatimiza miezi yake ya kuzaliwa.

Kitaalamu, mtoto njiti (premature indent), akiwa na umri kabla ya wiki 37 za ujauzito na kiafya anakuwa na uzito mdogo, uzito wa mtoto kwa kutotimiza miezi tisa.

Hulka yake kiafya, anakuwa na nywele mwilini, anapumua kusiko kawaida na kwa nguvu nyingi. Inaelezwa kuwa wanawake, wengi wenye historia ya kupata uchungu mapema, wapo katika hatari ya kujifungua njiti, ikilinganishwa na wasio na historia hiyo.

Sababu nyingine, inatajwa kuwa mjamzito anajifungua watoto zaidi ya mmoja, husababisha kupatikana watoto njiti.

Katika tafiti mbalimbali ambazo zimefanywa zinaonyesha, kuwa nusu ya watoto ambao huzaliwa mapacha wanakuwa njiti, ikilinganishwa na amezaliwa peke yake.

Ripoti ya Umoja wa Mataifa, Mei 10 kwa dhidi ya kuzaliwa kabla ya wakati, iliyotolewa na Shirika la Umoja la Afya Duniani (WHO) na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), inajumuisha makadirio yaliyoboreshwa na wanazuoni wa Uingereza, taasisi, London School of Hygiene and Tropical Medicine.



Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu. **PICHA: MTANDAO**

Kuhusu uwapo wa watoto wanaozaliwa kabla ya wakati, unagundua viwango vya kuzaliwa kabla ya wakati havijabadilika katika eneo lolote duniani katika muongo uliopita na watoto milioni 152 walio katika mazingira hatarishi walizaliwa hivi karibuni kutoka mwaka 2010 hadi mwaka 2020.

Kuzaliwa kabla ya wakati sasa ndio sababu kuu ya vifo vya watoto, ikichukua zaidi ya kifo kimoja kati ya vitano vya watoto vinavyotokea kabla ya kutimiza umri wa miaka mitano, baada ya kuzaliwa.

Watoto njiti wanaonusurika wanaweza kukabiliwa na changamoto ya afya ya maisha yote, pamoja na kuongezeka kwa uwezekano wa ulemavu na ucheleweshaji wa maendeleo.

**PENGO LA USAWA**

Inaelezwa kuwa wanawake walio na umri chini ya miaka 18, wapo hatarini kupata watoto njiti kwa kuwa kipindi hicho mfumo wa uzazi unakuwa haujakomaa.

Ni wanawake walio na umri unaozidi miaka 35 wapo hatarini, kwa sababu katika umri huo mkubwa wengi wao huwa na maradhi chochezi, kama kisukari na shinikizo la damu.

> **Asilimia 70 ya watoto njiti wanafariki ndani ya saa 48, kama hawajapata huduma sahihi kwa wakati.**

Inaelezwa kuteswa katika kipindi cha ujauzito ikiwamo na mawazo, nayo ni sehemu ya sababu ya kuzaliwa mtoto njiti.

Hivi karibuni, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, akasema takriban watoto 200,000 mpaka 300,000 kwa mwaka, wanazaliwa kabla ya mudaTanzania.

Anasema hayo, wakati wa maandalizi ya kuelekea awamu ya pili ya ugawaji vifaa tiba, kwa ajili ya huduma kwa watoto wanaozaliwa kabla ya muda katika hospitali zaidi ya 80 nchini.

Ummy anaongeza kuwa, asilimia 70 ya watoto njiti wanafariki ndani ya saa 48, kama hawajapata huduma sahihi kwa wakati.

Anabainisha kuwa juhudi zinazofanywa na Rais Dk. Samia, ni kuwezesha kupatikana vifaa tiba vyote muhimu vya kuwahudumia njiti nchini.

"Hospitali zilizokuwa zinatoa huduma za uangalizi kwa watoto njiti ni 14 tu, lakini kwa sasa zipo Hospitali Zenye Wodi za Watoto Njiti (NICU), zaidi ya 180 nchini, haya ni maendeleo makubwa hapa nchini," anasema.

Pia, anasema katika miaka minne iliyopita, huduma za uangalizi maalum kwa watoto njiti zilikuwa zinatolewa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), pia katika hospitali za rufani za kanda.

Kwa sasa huduma hizi zipo katika hospitali zote za rufani za mikoa mpaka ngazi za hospitali za wilaya ambapo jumla ni takriban hospitali 180 zinazotoa huduma hizo.

# Miaka 15 ya Mpango Afya ya Msingi, makubwa zamu ya Rais Samia

**INATOKA UK.11**

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, anamuunga mkono akiwa na rai kwa kamati hiyo, kudumisha utamaduni wa kutembelea hospitali na taasisi zilizo chini ya Wizara ya Afya, kushuhudia uwekezaji unaofanywa na serikali kwenye eneo la afya, katika MAMM zama za Rais Dk. Samia.

**HATUA ILIKOPIGA**

Ni Julai mwaka huu, ikiwa ni sehemu ya kuboresha mahitaji ya MAMM, pia mpango wa elimu kwa sekondari na msingi (MMEM na MMES),Dk.Samia akaridhia kibali kuajiri watumishi 21,200 wa kada za ualimu na afya.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Angellah Kairuki, anawataja katika mgawanyiko wa watumishi wa afya 8,070 watakotumikia hospitali za halmashauri mbalimbali, vituo vya afya na zahanati.

Pia, takwimu za afya, kupitia tovuti ya TAMISEMI, zinamuonyesha Dk. Samia Suluhu Hassan amewekeza katika Huduma za Dharura(EMD) 80 na Huduma za Wagonjwa Mahututi (ICU) 28 katika afya ya msingi na zimekamilika, sasa zinatoa huduma kwa wananchi.

Naibu Katibu Mkuu,TAMISEMI, Dk. Charles Mahera, anasema kwa watumishi wa sekta ya afya mkoani Njombe, kuna jengo la wagonjwa wa dharura katika Hospitali ya Wilaya ya Makete, ikiwa ni miongoni mwa majengo 80 chini ya uwekezaji wake, Rais, Dk. Samia



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Angellah Kairuki.

Dk. Mahera anasema, pia kuna magari 316 ya kubeba wagonjwa yatakayosambazwa katika huduma za afya ya msingi, ili kutoa huduma bora kunapotokea rufani ya haraka.

Aidha, anawataka maofisa ustawi wa jamii ,kwa kuzingatia utamaduni, miongozo na elimu ya lishe, ili kuondoa udumavu katika maeneo yao ya kazi.

Dk. Mahera anawatamkia maofisa afya nchini, katika kutekeleza malengo ya zama za 'Kazi Iendelee' akisema: "Fanyeni kazi yenu vizuri kwa kutoa elimu kwa ajili ya kuzuia magonjwa ya mlipuko kama vile kipindupindu...tutoe elimu kwa wananchi tusiwaache wenyewe."

"Hivi sasa vifaa vingi serikali imewekeza katika ngazi ya msingi, hivyo ni wakati wa kushirikiana na hospitali za mikoa kuwajengea uwezo watumishi wa ngazi ya msingi, ili vifaa vilivyowekezwa kuleta tija kwa kutoa huduma kwa wananchi," anaeleza.

Pia, anasisitiza hospitali za wilaya,vituo vya afya na zahanati kuwa na utamaduni wa kufanya ukaguzi wa dawa, vifaa tiba na ubora wa huduma ili kubaini matumizi sahihi ya uwekezaji wa rais, uliofanyika katika maeneo hayo.

Dk. Mahera anawaelekeza waganga wakuu wa wilaya nchini kusimamia kwa karibu Waratibu Programu kama Mfuko wa Kimataifa (Global Fund) na kuhakikisha fedha za programu hizo zinatumika kama zilivyopangwa na kwa wakati ili kuleta tija kwa wananchi.

AFYA

# Wachimba madini kinamama wanaowezesha kuwapo zahanati inayowatibu kijijini kwao

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

***ALHAMISI wiki iliyopita, safu hii ilikuwa na makala namna miradi, katika msitu unaotunzwa kijijini ukawezesha kupatikana zahanati, huko Namtumbo, Ruvuma. Katika hali kama hiyo Kahama, mkoani Shinyanga, kinamama wachimba madini nao wamewezesha mradi wa zahanati. Fuatilia...***

Kihistoria, uchimbaji madini kwa wanawake ulichukuliwa tofauti na wanaume, kinamama walionekana dhaifu na hawawezi kufanya shughuli nzito, zikiwamo za kuingia mashimoni.

Pia, imani potofu kwa hali zao za kimaumbile, ikionaishwa na namna madini yanavyopatikana, ikisababisha ugumu kwao kushirikishwa katika shughuli za uchimbaji wa moja kwa moja, badala yake wakawa wapishi wa vyakula na kufanya biashara ndogo za vinywaji migodini.

Baada ya kupatikana elimu katika kundi hilo, taratibu zikaanza kwao za uchenjuaji mchanga, ambao umeshatumika ili kupata fedha za kuendesha maisha na familia zao, hata wakapata hamasa ya kuingia mashimoni na kutaka kuchimba madini, kama lilivyo kundi la wanaume.

Wastani wa takwimu hadi sasa, wanawake ni asilimia 25 ya wachimbaji wadogo wa madini na kwenye muundo wa umiliki, wako asilimia 10 ya wamiliki leseni za madini.

Inatajwa hali hiyo inakaribisha haja ya kuendelea kuwekwa mazingira wezeshi ya kuongeza ushiriki wao, pia umiliki katika sekta ya madini. Kwa kutambua jitahada zao, serikali kupitia Wizara ya Madini, ilianzisha Chama cha Wachimbaji Wadogo Wanawake Tanzania (TAWOMA,) kinachowasimamia wachimbaji hao nchi nzima, hapo imo mgodi mdogo wa Nyamishiga.

Kwa kutambulika kwao, serikali ikaupatia usimamizi wa mgodi mdogo wa Nyamishiga uliopo kata ya Lunguya, Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga.

Kikundi cha Mashikamano Mining Group kimepiga hatua ya kukusanya maduhuli ya serikali zaidi ya shilingi bilioni mbili kwa muda mfupi, kulinganisha na mengine.

Hadi sasa kimekamilisha ujenzi wa zahanati kijijini Nyamishiga, kuhudumia wananchi na wachimbaji kwenye changamoto za kiafya, ikiendana na kununua samani za ndani, gari la wagonjwa litalotumiwa pia na vituo vya afya jirani.




Hafla ya kukabidhi gari la wagonjwa na zahanati, itokanayo na mchango wa wachimbaji wadogo. **PICHA SHABAN NJIA**

> **Utitiri wa kodi unasababisha uzalishaji kuwa mdogo na serikali kukosa mapato yake, fedha zinazopatikana zinaelekezwa katika kutatua changamoto katika sekta mbalimbali ikiwemo afya, elimu na maji.**

### WENYEJI WANAVYONENA

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Lungua, katika Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga Teddy Jacob, anasema kuna jumla ya wakazi 4,970 wa kijiji cha Nyamishiga wataondokana na adha ya kutembea umbali wa kilomita 10 kufuata matibabu katika Kituo cha Afya Lunguya, baada ya wachimbaji kukamilisha zahanati na kuikabidhi serikali, kianze kazi.

Kwa mujibu wa Jacob, kabla ya ukamilishaji, wananchi walikutana na kuchangishana fedha za ujenzi wa awali wa zahanati tangu mwaka 2018, wakapata Sh. milioni 23.5 wakajenga boma la kuhudumia wagonjwa wa nje (OPD).

Ni fedha zilichangishwa kupitia mfuko wa jeshi la jadi maarufu kama sungusungu mpaka pale wachimbaji walipolikamilisha.

Jacob anaeleza walipokea Sh. milioni 120, kutoka kikundi hicho kwa ajili ya ukamilishaji zahanati, kati ya hizo Sh. Milioni 198.53 zilitumika kukamilisha ujenzi wake, kujenga vyoo vya kisasa, kuchoma taka, nyumba ya mganga na kujengwa mfumo wa kuvuna maji ya mvua yatakayotumika kituoni, hasa kwa wajawazito wakati wa kujifungua.

"Kijiji chetu cha Nyamishiga kina wakazi 4,970 kilikuwa hakina zahanati na walilazimika kutembea umbali mrefu, wajawazito walijifungulia njiani kwa uwepo wa umbali huo.

"Ila sasa, tatizo hilo limetatuliwa na kikundi cha wachimbaji wanawake na jumla ya shilingi milioni 312.53 zimetumika," anasema Jacob.

Mkazi wa kijiji hicho, Rebeka William, anachangia hoja hiyo, kwamba wamekuwa wakilazimika kutembea umbali mrefu kilomita 10 kutafuta matibabu, vilevile katika kipindi cha masika, barabara zinaharibika hata kusababisha pikipiki na magari kushindwa kufika.

Ni hali inayowalazimisha kuhamia matumizi ya baiskeli na machela zinazovutwa na wanyamakazi, kama punda.

Anasema ni kipindi ambacho gharama za usafiri zinapanda mara mbili kwa pikipiki ni shilingi 10,000 badala ya shilingi 5,000 na kwa wasiokuwa na uwezo wa kumudu gharama hizo hususani wajawazito, wamekuwa wakilazimika kujifungulia majumbani.

Kwa mujibu wa Rebeka, wale wanaojitahidi kufikia kwenye kituo tajwa cha afya, wanapochelewa wamekuwa wakihatarisha usalama wao na watoto.

### KIKUNDI CHA MADINI

Mwenyeikiti wa Kikundi cha Mshikamano Mining Group Semeni Malale, anasema wamekabidhi gari la wagonjwa lenye thamani ya shilingi milioni 75 litalotumika hapo na vituo vya afya jirani.

Malale anasema, wamenunua pia samani ndani ya zahanati hiyo kwa thamani ya shilingi milioni nne, hali kadhalika kutolewa madawati 100 kwa Shule ya Msingi Nyamishiga, akiwataka wadau wa afya kuiga mfano huo.

### MTAZAMO SERIKALINI

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Msalala, Flora Sagasaga, anaitaja kuwa hatua inayopaswa kuigwa na wachimbaji wengine kuwezesha kuwapo huduma muhimu kaika maeneo wanakoishi.

Anasema, asilimia 80 ya mapato ya ndani ya halmashauri hiyo, inatokana na madini hasa kwa wachimbaji wadogo, hivyo watadumisha mazingira rafiki yanayoongeza uzalishaji mapato watayoyaelekeza katika sekta ya afya, elimu na huduma ya maji, ili kukabiliana na maradhi kwa wachimbaji hao.

Mkuu wa Mkoa Shinyanga, Christina Mndeme, anakipongeza kikundi hicho kwa kukamilisha ujenzi wa zahanati iliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi tangu mwaka 2018 na mpaka sasa inaelekea kuanza kutoa huduma, kwamba serikali imeendelea kushirikina na wadau wa afya kusogeza huduma karibu na wananchi.

Anasema, mkoa huo umepokea Sh. bilioni 26 za kuboresha huduma katika sekta ya afya na sasa dawa zinapatikana kwa asilimia 90 katika zahanati, vituo vya afya na hospitali. Zahanati hiyo itaanza kutoa huduma mara moja ili kuwaondolea adha wananchi kutembea umbali huo na wachimbaji pia.

Waziri wa Madini Dk. Doto Biteko anakipongeza kikundi, pia kwa kukusanya maduhuli ya serikali zaidi ya Sh. bilioni 2 na kukabidhi zahanati ya Kijiji, pia gari la wagonjwa serikalini, kuwahudumia wananchi wanaowazunguka, kukabili vifo vitokanavyo na uzazi, akivitaka vikundi vingine kuiga mfano huo.

Anaongeza, kwa sasa wanaendelea kukamilisha taratibu za kisheria, ili kikundi hicho kiweze kukabidhiwa leseni ya uchimbaji madini.

Kwa mujbu wa Waziri Biteko, anapongeza vikundi vya wanawake, kwa sababu vinafanya mambo makubwa, kulinganisha hata vya kinababa vilivyoko.

Dk. Biteko anawataka wakurugenzi wa halmashauri zote nchini, ambazo zina wachimbaji wadogo, kuacha tabia ya kulimbikiza utitiri wa kodi dhidi yao na badala yake watoze kodi zilizopo kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za madini, ili kuongeza uzalishaji na serikali kupata mapato yake.

"Utitiri wa kodi unasababisha uzalishaji kuwa mdogo na serikali kukosa mapato yake, fedha zinazopatikana zinaelekezwa katika kutatua changamoto katika sekta mbalimbali ikiwemo afya, elimu na maji.

"Hivyo, tutoze kodi zilizopo kisheria ili waone umuhimu wake na wasiingie tamaa ya kutorosha madini yetu," anaongeza Dk. Biteko.





# WMA yatoa maagizo wauzaji mitungi ya gesi nyumbani

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAKALA wa Vipimo (WMA) umewataka wauzaji wa mitungi ya gesi inayotumika majumbani kwa ajili ya kupikia kuwa na mizani itakayotumika kupima ujazo halisi ili kuondokana na malalamiko ya wananchi kutapeliwa.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa wakala huo, Stella Kahwa alitoa maagizo hayo jana jijini hapa, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya wakala huo na mwelekeo wa mwaka wa fedha 2023/24.

Kahwa, alisema kumekuwepo na malalamiko mengi kutoka kwa wananchi kutapeliwa kiasi kinachouzwa kwenye mitungi ya gesi kuwa tofauti na ujazo halisi uliondikwa.

"Kuna watu wanalalamika kuwa wananunua mtungi wa gesi lakini wanautumia kwa muda wa siku mbili hali ambayo ni kinyume na sheria za wakala huu lazima wauzaji wote wawe na mizani kwa ajili ya kupima ujazo wa gesi lakini pia mizani kwa ajili ya kupima uzito wa mtungi wenyewe ili mteja ajue ni kilo ngapi kanunua"alisema Kahwa.

Aidha, alisema muuzaji kupima mtungi wa gesi kabla hajamuuzia mteja ni suala la lazima siyo hiyari na mteja anapaswa kuhakikisha kuwa bidhaa alionunua inaujazo halisi uliotakiwa na siyo vinginevyo.

Akizungumzia majukumu ya wakala huo alisema jukumu la kusimamia kiasi cha gesi inayoingia nchini kwa meli zitokazo nje ya nchi ili kujua kiasi cha gesi hiyo (LPG) iliyoagizwa na wafanyabiashara ili kujiridhisha kuwa wanunuzi wa bidhaa hiyo wanapata kiasi sahihi kulingana na thamani ya fedha iliyolipwa.

Kadhalika, alisema pamoja kuhakiki kiasi cha gesi toka nje ya nchi pia wanafanya ukaguzi na uhakiki wa mitungi ya gesi ya ujazo tofautitofauti ili kuhakikisha kuwa wanunuzi wa gesi hiyo ya kupikia majumbani wanapata kiasi sahihi kulingana na thamani ya fedha waliyolipa,

Katika sekta ya maji alisema WMA kwa sasa unafanya uhakiki wa dira zote za maji zinazotumiwa na mamlaka za maji kwa wateja wao.

"Uhakiki unafanywa kwa dira zote mpya na zile ambazo tayari zipo katika matumizi ili kuhakikisha mamlaka za maji zinapata tozo sahihi kwa maji yaliyotumiwa na mteja na mteja nae analipa gharama sahihi kulingana na maji aliyoyatumia"alisema

Alisema uhakiki wa dira hizo ni sehemu ya mambo ya msingi yanayochangia katika utekelezaji wa ilani ya chama tawala kwa kuhakikisha huduma ya maji safi na salama inaendelea kuimarishwa na kuwafikia wananchi kwa zaidi ya asilimia 85 ya wakazi wa vijijini na zaidi ya asilimia 95 kwa mijini ifikapo mwaka 2025.

"Uhakiki wa dira za maji ulianza rasmi Machi, 2019 na hadi Juni, 2023, wakala umefanikiwa kuhakiki jumla ya dira za maji 420,497 kutoka kwenye mamlaka mbalimbali za maji nchini" alisema.

Alisema kwa upande wa usafiri wa anga, wakala huo umeendelea kuhakiki mizani yote inayotumika kwenye viwanja vya ndege ili kuwa na uhakika wa kiasi cha uzito ili kuepusha kupata ajali kutokana na uzito mkubwa.

Alisema: "Pamoja na mizani hiyo ya kwenye viwanja vya ndege, wakala umeendelea kuhakiki mita za tangi na mita za mafuta zinazotumika kuweka mafuta kwenye ndege ili kuhakikisha mafuta yanawekwa kwenye ndege hizo ni sahihi kulingana na uwezo wa ndege husika".





Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), Bahati Geuzye (wa pili kulia) na Mkurugenzi wa Baobab Shalom Ltd, Yev Semikov (wa pili kushoto) wakisaini makubaliano ya ushirikiano kwa ajili ya kugawa majarida 700 ya OYLA Africa, yanayohimiza wanafunzi kusoma masomo ya Sayansi, Teknolojia na Hisabati katika hafla fupi, jijini Dodoma juzi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Wataalamu TEHAMA watakiwa kufanyia kazi mifumo ya taarifa

**Na Paul Mbeja,** DODOMA

KATIBU Mkuu Wizara ya Afya, Dk. Seif Shekalaghe amewataka wataalam wa TEHAMA kufanyia kazi mifumo ya taarifa ya wizara isomane na mifumo mingine serikalini, kuleta tija na kurahisisha utoaji wa huduma nchini.

Aliyasema hayo juzi alipokuwa akifungua kituo cha umahiri katika masuala ya afya kidijitali jijini hapa.

Alisema kituo hicho ni utekelezaji wa maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan ambao aliagiza kuanza kwa matumizi ya tiba mtandao lakini pia ameelekeza lazima mifumo yao ipungue.

"Ninafurahi siku ya leo ni moja ya hatua ya utekelezaji wa maelekezo ya Rais. Wataalam wetu wakikaa hapa wataweza kuja na suluhisho la changamoto za mifumo iliyopo na kuwa na mifumo michache yenye tija," alisema Dk. Shekalaghe.

Alisema kituo hicho cha umahiri katika masuala ya kidijitali (CDH) kitasaidia kuunganisha mifumo ya sekta ya afya pamoja na kupunguza mifumo iliyopo katika Wizara ya Afya.

Vilevile, Dk. Shekalaghe alisema kuwa taarifa zinazotolewa na kituo hicho ziweze kutumika kwa ajili ya utafiti utakaosaidia kufanya maamuzi mazuri zaidi.

Naye, Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Kimataifa la PATH, Amos Kamugisha alisema wamewezesha ukarabati wa kituo hicho kuweka samani pamoja na vifaa vya teknolojia.

Alisema moja ya umuhimu wa kituo hicho ni kutengeneza mifumo ambayo inazungumza na kupunguza mifumo mingi iliyopo katika sekta ya afya kwa sasa.

Kaimu Mkurugenzi wa TEHAMA Wizara ya Afya, Silvanus Ilomo amesema kuwa kituo hicho kitatumiwa sio tu na Wizara ya Afya bali wataalam wengine wa sekta ya afya kwa ajili ya kukutana na kuja na mifumo yenye tija katika uboreshaji wa huduma za afya nchini.

## Asali, bidhaa za mbao kuingizwa mfumo stakabadhi ghalani

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BODI ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala imesema inatarajia kuingiza kwenye mfumo wa stakabadhi ghalani asali na bidhaa za mbao.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa bodi hiyo, Asangye Bangu alibainisha hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mfumo huo kwa mwaka 2022/23 na mwenendo wa mwaka 2023/24.

Alisema wanatarajia kuingiza bidhaa za mbao kwa upande wa misitu hususani kwa Mkoa wa Njombe na elimu imetolewa kwa uongozi na vikundi vya wafanyabiashara ya mbao ili kujenga uelewa wa pamoja juu ya utekelezaji wa mfumo.

"Bodi inaendelea na maandalizi ya kuingiza asali hususani katika Mkoa wa Tabora, kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge. Hii itasaidia kuleta ushindani wa wanunuzi hivyo kuchochea bei na kuongeza ubora wa zao,"alisema.

Aidha, alisema hadi kufikia Juni 30, mwaka huu kilogramu milioni 370.7 za mazao 13 yameuzwa kupitia mfumo wa stakabadhi za ghala hapa nchini zenye wastani wa Sh.bilioni 741.5 Alitaja mazao hayo ni soya, mbaazi, ufuta, dengu, korosho, karanga, mahindi, maharage, mhogo, mchele, mpunga na mtama.

Alisema mfumo huo umewezesha Sh.bilioni 22.24 kupelekwa serikalini kupitia halmashauri zao kwenye mikoa iliyotekeleza mfumo huo.

Alisema wakulima wengi nchini wamekuwa na shauku ya kutaka kufahamu jinsi mfumo unavyofanya kazi na hivyo kupelekea kujiuliza maswali mengi.

Pia alisema bodi imeendelea kupeleka mfumo katika maeneo ya kanda zote nchini kwa bidhaa mbalimbali kwa kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Soko la Bidhaa Tanzania kwa pamoja wamekamilisha mwongozo wa mauzo ya mazao jamii ya kunde ikiwamo soya, dengu, mbaazi na choroko.

Alisema mfumo huo tayari umeanza kutumika katika mikoa ya Lindi, Mtwara, Ruvuma, Tanga, Morogoro na Manyara.





# Wananchi 500 kufanyiwa upasuaji mtoto wa jicho bure

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

KAMBI maalumu kwa ajili ya matibabu ya macho kwa wananchi imezinduliwa wilayani Mbarali katika Mkoa wa Mbeya, ambapo zaidi ya watu 500 wanatarajiwa kufanyiwa upasuaji wa mtoto wa jicho.

Kambi hiyo ilizinduliwa jana na Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Kanali Denis Mwila ambapo kambi hiyo imeandaliwa kwa ushirikiano kati ya serikali na shirika lisilokuwa la kiserikali la Keller International.

Meneja wa shirika hilo, Athuman Tawaqual alisema kambi hiyo ni ya nne ikitanguliwa na ya awali ambayo ilikuwa kwa ajili vikope na kwamba ya sasa hivi ni kwa ajili ya mtoto wa jicho pekee.

Tawaqual alisema kabla ya kambi hiyo walianza katika Mkoa wa Songwe ambako walikuwa wanafanya upasuaji katika Hospitali ya Wilaya ya Songwe Mwambani ambako waliwafanyia upasuaji wananchi 270.

Alisema wagonjwa wote wanaopata huduma hiyo hawalipi chochote na badala yake wanagharimiwa kila kitu kuanzia uchunguzi, usafiri, dawa na hata upasuaji.

Alisema gharama za upasuaji wa jicho moja ni Sh. 200,000 gharama ambazo wananchi wa kawaida hawawezi kumudu kutokana na hali ya uchumi walionao.

"Tunaishukuru serikali kupitia Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa ushirikiano mkubwa kuwezesha kufanikisha zoezi hili," alisema Tawaqual.

Alisema pamoja na kugharamia matibabu kwa wagonjwa pia shirika hilo linawajengea uwezo madaktari na wauguzi ili wawe na utaalamu wa kutoa huduma hizo baada ya mradi kufikia ukomo.

Meneja Mpango wa Taifa wa Huduma za Macho kutoka Wizara ya Afya, Dk. Bernadetha Shilio alilishukuru Shirika la Helen Keller kwa kufadhili kambi hiyo na kulipia gharama zote kwa wagonjwa.

Dk. Bernadetha alisema kambi hiyo ilianza Agosti 14 mwaka huu na inatarajiwa kuendelea wiki nzima na kwamba ufuatiliaji utafanyika nyumba kwa nyumba ili kubaini wagonjwa wote wenye tatizo la mtoto wa jicho.

Alisema mpaka sasa wamewafikia wagonjwa 800 wenye matatizo ya macho lakini wanaostahili kufanyiwa upasuaji wa mtoto wa jicho ni 500 na kwamba baadhi yao wanatakiwa kufanyiwa upasuaji macho yote mawili.

"Huduma hii ni ya kipekee kidogo kwa sababu wagonjwa hawa wanatafutwa kwenye nyumba zao wakipatikana wanafanyiwa uchunguzi wa awali halafu wanakuja kwenye kambi kufanyiwa matibabu hasa upasuaji," alisema Dk. Bernadetha.

Alisema tangu upasuaji huo umeanza zaidi ya asilimia 80 ya wagonjwa wanapata matokeo mazuri kwa macho yao kuanza kuona kama ilivyokuwa kabla hawajapata matatizo hayo.

Mwakilishi wa Mratibu wa Macho kutoka TAMISEMI, Ernest Paul alisema serikali imetoa Sh. milioni 50 katika kila halmashauri nchini ili kuboresha huduma za macho katika ngazi ya msingi.

Alitoa wito kwa wakazi wa Wilaya ya Mbarali kujitokeza kwa wingi na kupatiwa huduma ya upasuaji wa mtoto wa jicho ili kuepuka ulemavu wa kutokuona.

Jema Gidala mkazi wa Mwatenga Wilaya ya Mbarali aliishukuru serikali pamoja na Shirika la Helen Keller International kwa kutoa huduma hiyo bure akieleza kuwa alikuwa hana uwezo wa kugharamia. Alisema kabla ya kupata huduma hiyo aliamini kwamba asingeweza kuona tena kutokana na hali ya macho yake ilivyokuwa.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Kanali Mwila aliwataka wananchi wa wilaya hiyo kujitokeza kupima ili wakibainika kuwa na matatizo hayo watibiwe mapema.



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (wa pili kulia), akikabidhi taulo za kike kwa wanafunzi wa shule za sekondari za Halmashauri ya Jiji la Mbeya juzi, zilizonunuliwa na halmashauri hiyo kwa kutumia mapato ya ndani. Kulia ni Meya wa Jiji hilo, Sheikh Dor-Mohamed Issa. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## TAKUKURU yabaini upungufu kwenye miradi ya bil.127/-

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Mbeya, imebaini upungufu kwenye utekelezaji wa miradi 13 yenye thamani ya Sh. bilioni 127.6

Mkuu wa TAKUKURU wa Mkoa wa Mbeya, Vangsada Mkalimoto aliyasema hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji majukumu ya taasisi hiyo katika kipindi cha miezi mitatu.

Alisema miradi waliyochunguza inahusu idara mbalimbali ikiwemo ujenzi wa majengo ya serikali, miradi ya umwagiliaji, miradi ya maji pamoja na barabara mbalimbali za ndani ya mkoa huo.

Moja kati ya miradi ambayo aliitaja kuwa na mapungufu ni pamoja na ujenzi wa Jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ambalo limegharimu Sh. bilioni 2.7

Alisema mradi huo uko katika hatua za umaliziaji lakini kwa mujibu wa mkataba ulitatakiwa uwe umekamilika na kwamba umechelewa kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ucheleweshaji wa fedha kutoka TAMISEMI.

"Tumeshauri usimamizi wa mradi huo uwe wa karibu ili ukamilike na kuanza kutumika kama ilivyokusudiwa, kwa mujibu wa mkataba ulitakiwa uwe umekamilika tangu Juni 2023," alisema Mkalimoto.

Aliutaja mradi mwingine kuwa ni wa maji wa chanzo cha Mto Kiwira ambao unatekelezwa na Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-WSSA) ambao unagharimu Sh. bilioni 99.6.

Alisema kwa mujibu wa mkataba wa mradi huo mkandarasi alitakiwa awe amepeleka vifaa vya kazi na kujenga kambi lakini mpaka sasa hakuna kilichofanyika.

Hivyo, alishauri wasimamizi wa miradi hiyo kuhakikisha wanaisimamia kwa ukaribu ili itekelezwe na kukamilika kwa muda ulio-

# Wanafunzi washukuru kujengewa mabweni, vyoo na madarasa

**Na Elizabeth John,** NJOMBE.

WANAFUNZI wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Makete ya mkoani Njombe, wameishukuru serikali kwa kuwaboreshea mazingira ya kusomea ikiwemo ujenzi wa mabweni, madarasa na vyoo.

Waliyasema hayo wakati wa ziara ya Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka iliyokuwa na lengo la kukagua maendeleo ya shule pamoja na kuangalia taarifa za wanafunzi wa kidato cha tano kuripoti shuleni.

Mmoja wa wanafunzi hao, Tamasha Eliud ambaye ni mwanafunzi wa kidato cha sita alisema uboreshwaji wa miundombinu utasaidia kuongeza idadi ya wasichana katika shule yao na hivyo kuongeza kiwango cha elimu.

"Zamani wasichana walikuwa hawapewi nafasi ya kupata elimu lakini sasa hivi miundombinu imeongezeka wanafunzi wa kike wanazidi kuongezeka kupata elimu ambayo itasaidia katika kuwaelimisha wanajamii wengine ambao utamaduni kwamba wasichana hawawezi"alisema Tamasha.

Naye Queen Chengula mwanafunzi kidato cha tatu alisema wakati uliopita walikuwa na majengo machache lakini walivumilia.

Makurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Makete, William Makufwe, alisema Sh. bilioni 2.5 zimeletwa kwa ajili ya ujenzi wa mabweni na madarasa ili kuondoa changamoto ya mlundikano wa wanafunzi wa kidato cha tano katika wilaya hiyo.

Awali Mkuu wa Shule hiyo, Sayuni Sanga, alisema tayari wanafunzi 87 wa kidato cha tano wameshariipoti shuleni hapo kati ya 454, huku wengine wakiendelea kuwasili.

Mkuu wa Wilaya ya Makete, Juma Sweda alisema licha ya wanafunzi wengi kupangiwa katika shule hiyo lakini watahakikisha wote wanaripoti na kuanza msomo.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka, aliwasisitiza wanafunzi ambao hawajaripoti shuleni hadi sasa kufanya haraka kwani shule hiyo imekuwa na kiwango bora kitaaluma ukilinganisha na shule nyingine.



## HABARI ZANZIBAR

# Ndege kolokolo domo refu hatarini kutoweka

**Na Rahma Suleiman, aliyekua** MUHEZA

KAIMU Mhifadhi wa Hifadhi ya Msitu wa Amani-Niro, Alphonce Nyululu, amesema ndege aina ya kolokolo domo refu, wako hatarini kutoweka nchini.

Amesema ndege hao ambao ni adimu duniani, kwa Tanzania anapatikana kwenye safu ya Milima ya Usambara Mashariki kwenye hifadhi hiyo wilayani Muheza mkoani Tanga.

Amesema hifadhi ya msitu huo ina ndege zaidi ya 340 na ndege huyo kwa sasa yupo hatarini kutoweka, hivyo anahitaji kulindwa. Aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari kutoka Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JETI) waliotembelea hifadhi ya msitu huo, chini ya ufadhili wa USAID Tuhifadhi Maliasili.

Alisema ndege huyo anafaida nyingi lakini ni kivutio kikubwa cha watalii katika hifadhi hiyo, kwamba ili asitoweke kunahitajika nguvu za ziada.

Alisema kuanzia mwaka 2007 hadi 2023 hifadhi hiyo imeingiza Sh. milioni 538.0 baada ya kupokea watalii 14,096 waliokuja kufanya utalii katika hifadhi hiyo ikiwemo utalii wa ndege huyo.

Alisema wananchi wanafaidika na uwepo wa msitu huo ambao umezungukwa na vijiji 20 na kuna baadhi ya fedha asilimia 20 zinazotokana na utalii wanapewa kwa ajili ya shughuli za maendeleo.Nyululu alisema hifadhi hiyo imeanzishwa mwaka 1997 lengo ni kulinda, kuhifadhi na kuhakikisha bayoanuai zote zinahifadhiwa vizuri na hifadhi hiyo ni tegemeo kubwa kwa Jiji la Tanga kwa ajili ya kupata maji. Mtafiti wa ndege kutoka shirika lisilo la kiserikali linalohusika na uhifadhi wa ndege na mazingira Tanzania (Nature Tanzania), Edigar Apolinary, aliwataka wananchi wanaozunguka msitu huo kutokata miti wala kuchoma moto mashamba yao ili ndege huyo asitoweke.

Alisema shirika la Nature Tanzania, linaendelea kutoa elimu kwa wanafunzi wa shule kuhusu umuhimu wa ndege ambapo wamekuwa na uelewa na kuwatambua ndege wa aina mbalimbali.



Wanafunzi wa shule ya sekondari ya Shebomeza, wilayani Muheza, mkoani Tanga, wakiwa katika somo la vitendo la kuangalia ndege kwa tumia kifaa maalum katika msitu wa hifadhi Amani wilayani humo hivi karibuni. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Kampuni 100 kushiriki maonyesho utabibu, maabara

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI zaidi ya 100 kutoka ndani na nje ya nchi zinatarajiwa kushiriki kwenye maonyesho ya pili ya kimataifa ya utabibu na maabara yatakayoanza Agosti 24 hadi 26 jijini Dar es Salaam.

Maonyesho hayo yameandaliwa kwa pamoja na kampuni ya ETSIPL ya India, Wizara ya Afya pamoja na Chama cha Wafamasia Tanzania (PST).

Maonyesho hayo yanayofanyika mara ya pili hapa nchini yamelenga kutoa elimu ya dawa, matibabu, afya, upasuaji, maabara, mifupa na masuala mengine yanayohusu sekta ya afya kwa ujumla.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mkurugenzi wa ETSIPL, Vijayanka Brighuvanshi, alisema maonyesho hayo yatakutanisha wataalam katika sekta ya afya ambapo washiriki watapa fursa ya kubadilishana ujuzi na maarifa.

Aidha, Rais wa Chama cha Wafamasia Tanzania (PST), Fadhil Hezekiah, alisema mpaka sasa tayari kampuni 17 za Tanzania zimethibitisha kushiriki katika maonyesho hayo.

"Tunatarajia pia kampuni kutoka Kenya, India, China na Yemen ambapo kwa ujumla yatakuwa 105 yakiwemo hayo 17 kutoka hapa Tanzania," alisema Hezekiah.

Alisema nafasi bado ipo wazi kwa kampuni zingine za ndani na nje ya nchi yanayotaka kushiriki kwenye maonyeso hayo.

Hezekiah alisema kwa mwaka huu maonyesho hayo yanaungwa mkono na taasisi nyingine za Mamlaka ya Chakula na Dawa (TMDA), Chama cha Watoa Huduma Binafsi za Afya Tanzania (APHFTA), Chama cha Waigizaji wa Dawa za Binadamu (TAPI), Chama cha Wazalishaji wa Ndani wa Dawa za Binadamu (TPMA), Chama cha Madaktari Bingwa wa Upasuaji Tanzania (TSA) na Chama cha Madkatari Wanawake Tanzania (MEWATA).

# Serikali kutumia TEHAMA kuleta ufanisi, utoaji huduma

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI Mtendaji wa Wakala wa Serikali Mtandao, Said Seif Said, amesema lengo la serikali ni kuhakikisha wanatumia TEHAMA katika utendaji wa serikali ili kuleta ufanisi katika utoaji wa huduma.

Aliyasema hayo wakati akifungua kikao cha kujadili rasimu ya sera ya serikali mtandao na mpango mkakati wa serikali mtandao ulioshirikisha wakurugenzi wa mipango kutoka serikalini. Alisema ni lazima kwa watendaji hao kufanya kazi kwa karibu ili mambo yaweze kufanikishwa.

Mkurugenzi huyo alisema teknolojia hivi sasa zinabadilika, hivyo ni lazima kuziangalia kwa karibu ili kufaidika nazo.

Hivyo aliahidi kuwa kupitia serikali mtandao serikali itahakikisha inaendelea kuilinda mifumo hiyo na haichezewi na inaleta tija katika uchumi wa nchi.

Mwenyekiti wa Bodi wa Ushauri E- Goverment, Dk. Mzee Suleiman Mndewa, alisema wameanza safari ya mabadiliko, hivyo ni lazima kuwa na miongozo ambayo itasaidia katika kuleta mabadiliko ya TEHAMA nchini.

Hivyo, aliwataka watendaji kuacha tabia ya kufanya kazi kwa mazoea na badala yake kufanya kazi kwa bidiii na uadilifu ili kuisaidia serikali katika kufikia malengo ya kidijitali.

Naye Mdhadhiri kutoka Chuo cha Taifa Zanzibar (SUZA), Dk. Salim Suleiman, alisema serikali nyingi duniani zimebadilisha mifumo yake jinsi ya kufanya kazi na zinahama kutoka mifumo ya zamani na kuja katika mifumo mipya ambayo inarahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi.

# Uwekezaji wa hoteli za nyota tano wamfurahisha waziri

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, amesema kuongezeka kwa uwekezaji wa hoteli za kifahari kunathibitisha kukua zaidi kwa sekta ya utalii Zanzibar.

Aliyasema hayo juzi wakati akifungua Hoteli ya 'Double A' huko Nungwi Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Alisema serikali itaendelea kushirikiana na wawekezaji walio tayari kuiunga mkono Zanzibar katika kuinua sekta hiyo ambayo ndio muhimili mkuu wa uchumi kwa sasa.

Alisema ufunguzi wa hoteli hiyo ya kisasa unaakisi dhamira ya Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi, kuimarisha sekta ya utalii na hivyo kuongeza pato la taifa na kustawisha uchumi wa nchi.

Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud, alisema ongezeko la uwekezaji mkoani humo linatokana na usalama na amani iliyopo.

Aliahidi kuwa serikali ya mkoa itaendelea kuimarisha ulinzi na usalama na kuwataka wawekezaji na watalii wanaotembelea huko, wajisikie wako nyumbani.

Hata hivyo, alikiri kuwepo changamoto mbalimbali ikiwemo malalamiko ya wageni dhidi ya watembezaji watalii wasio rasmi pamoja na kelele za muziki wakati wa usiku.

"Unapozungumzia utalii jambo la kwanza ni usalama na ukikosekana sekta hiyo itayumba. Hivi karibuni nilifanya kikao na masheha nao wameshazungumza na ndugu zetu walinzi wa kimasai na 'Beach boys' wote, kuwahimiza kutii sheria bila shuruti, wakikaidi tutawaelekeza katika njia sahihi," alifafanua.

Mmiliki na Mkurugenzi wa hoteli hiyo Adrian Held kutoka Uswis, alisema uamuzi wa kununua bangaloo lililokuwa na vyumba tisa vya kienyeji na kujenga hoteli ya kisasa katika eneo hilo, ulitokana na kuvutiwa na haiba ya Zanzibar na ukarimu wa watu wake.

Alisema kuwa, mradi huo uliogharimu Dola milioni 2.8 na kujenga hoteli yenye vyumba 25 vya viwango vya aina tatu, umeajiri wafanyakazi 50 ambapo asilimia 95 ni Watanzania.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## DEED POLL OF A CHANGE OF NAME

**BY THIS DEED, I MARY AUGUSTINE MREMA** of P.O.Box 14611 Dar es Salaam **DO HEREBY** wholly absolutely and utterly renounce relinquish and abandon the use of my former names of **MARY PENDAELI SINGA** and **MARY AUGUSTINE** LYATONGA MREMA and adopt as from the date of this poll and in substitution of my former name, the name of **MARY AUGUSTINE MREMA.**

For the purpose of evidence of such determination I hereby declare that I shall at all times hereafter in all records, deeds documents and other writings and in all actions, suits and proceedings as well as in all public and private dealings and transactions and occasions whatsoever use and subscribe the said name of **MARY AUGUSTINE MREMA** as my name in lieu of and substitution for my former names of **MARY PENDAELI SINGA and MARY AUGUSTINE LYATONGA MREMA.**

I hereby expressly authorize and require all and every person and whatsoever at all times after the date hereof to designate, describe and address me by the name of **MARY AUGUSTINE MREMA.**

**IN WITNESS WHEREOF I** herein substitute my old names of **MARY PENDAELI SINGA** and **MARY AUGUSTINE LYATONGA MREMA** by the new name of **MARY AUGUSTINE MREMA** and have set my hand at Dar es Salaam this 30th day of August 2018



---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya TEMEKE**
**Kituo JUMUISHI**
**Mkoa DAR ES SALAAM**
**Usimamizi wa mirathi Na 1183/ 2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU JUMA MOHAMED MNKENI WA.........**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA AMINA HEMED JUMA**
**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa mirathi Mahakama za mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote / maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 19 mwezi 9 mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 14 Mwezi 8 Mwaka 2023

HAKIMU

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**WILAYA YA MOROGORO**
**KITUO CHA MJINI**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na......85/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: NUHU ISSA MUHAPA wa MAFISA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA CLARA SYLVESTER MHINA**
**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 24 Mwezi 08 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

Imetolewa leo tarehe 09 mwezi 08 mwaka 2023

---

## KUPOTEA KWA VYETI



**HALIMA HAMIS** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba : S0823-0055 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **THAQAAFA SECONDARY SCHOOL** mwaka **2013** na cheti cha kidato cha sita chenye index namba : S 2499-0620 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **TUSIIME SECONDARY SCHOOL** mwaka 2016. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: DOD/DOD/RB/229120/2023**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GLADNESS DANIEL GEHANDU** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA IST** yenye usajili namba: **T 823 DWF , CHASSIS NAMBA: NCP600228205 na ENGINE NAMBA: 2NZ8205.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: PHQ/ARU/ARU/90/2023**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA DAR ES SALAAM**
**TAXATION NO. 130 OF 2023**

**THE REGISTERRED TRUSTEES OF AL JUMAA ARAB MOSQUE & 4 OTHER..............................MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**ABDULKARIM RASHID ALLY &1 ANOTHER.........................................MJIBU MAOMBI**

**KWA: ABDULKARIM RASHID ALLY & 1 ANOTHER DAR ES SALAAM.**

**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa mdai aliyetajwa hapo juu amefungua maombi ya gharama za shauri Na Rufaa 130/2023 dhidi yako, unatakiwa kufika katika Mahakama hii tukufu wewe mwenyewe au wakili wako au mwakilishi wako anayetambulika kisheria tarehe 28/8/2023 saa 4:00 asubuhi mbele ya Mhe.S.B. FIMBO Naibu Msajili, kujibu madai dhidi yako.

Unaagizwa kuleta vielelezo vyote ambavyo unatarajia kuvitumia katika utetezi wako siku hiyo.

**Angalia:** Kama usipohudhuria siku hiyo iliyotajwa hapo juu, na Mahakama ikithibitisha kama umepokea wito huu, shauri litasikilizwa na kutolewa maamuzi bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa mkono wangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 16 Mwezi 8 2023.

THE HIGH COURT OF TANZANIA
**S.B. FIMBO**
**NAIBU MSAJILI**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**EMEC ENGINEERING CO. LTD** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba ya usajili : **T 407 BLL,** CHASSIS NAMBA: **TRJ-1205008655** na ENGINE NAMBA: **NnZTRFE .** kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/ILA/314/2023**

---

## KUPOTEA KWA VYETI



**RAMADHANI YUNUSI MMBAGA,** anatangaza kupotea kwa cheti chake Cha kidato Cha Nne na Kidato Cha Sita, Kidato Cha Nne index no **S2521-0050** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia Shule ya Mtakuja Sekondari Mwaka 2014.Kidato Cha Sita index no **S0320-0651** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia Shule ya Kigoma Sekondari Mwaka 2017. Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo cha Polisi.
TAARIFA YA POLISI: **PHQ /DOD/DOD/ 160/ 2023.**

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**
**Kituo cha CHAMWINO MJINI MKOA DODOMA**
**Usimamizi wa Mirathi Na 53/ 2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU IDOWA SELEMANI IDOWA WA MAILI MBILI**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA ABDILAH IDOWA SELEMANI**
**TANGAZO**
**Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 24 Mwezi 08 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia**
* Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuleta mahakamani kukaguliwa
* Marehemu hakuacha wosia
* Futa isiyohusika

Imetolewa leo tarehe 15 Mwezi 08 Mwaka 2023

..................
**Hakimu**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**SHARIFA MUSA BAKARI** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya **SANLG** yenye usajili namba **T 383 BAY, CHASSIS NAMBA: LBRSPJB5989038428 na ENGINE NAMBA: C8366582.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **ARU/LON/RB/144496/2023**

---

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 745 700 710***

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 0677020701**
**E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,**
**WEBSITE: WWW.IPPMEDIA.COM**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Viongozi Ecowas njia panda ACCRA

**ACCRA,** Ghana

VYANZO mbalimbali vya kijeshi vimesema wakuu wa majeshi kutoka nchi za Jumuiya ya Afrika Magharibi (ECOWAS) watakutana nchini Ghana, kwa ajili ya kujadili Niger.

Mkutano huo unaofanyika kwa siku mbili kuanzia leo, unafanyika baada ya ule wa wakuu wa majeshi wa nchi hizo wanachama uliotakiwa kufanyika mwishoni mwa wiki iliyopita kuahirishwa ghafla.

Mkutano huo unafanyika wiki moja baada ya marais wa jumuiya ya ECOWAS kuazimia kupeleka kikosi cha dharura cha kijeshi kumrejesha madarakani Mohamed Bazoum, ambaye alipinduliwa na jeshi.

Wakuu wa jumuiya hiyo walikutana katika mji wa Abuja nchini Nigeria Alhamis iliyopita na wote walionekana kubadili msimamo na kusisitiza malengo ya Jumuiya hiyo kutumia njia za kidiplomasia kuhusu kinachoendelea Niger.

Katika hatua nyingine, Rais wa Russia Vladimir Putin alizungumza kwa njia ya simu na Rais wa Mali Assimi Goïta, ambaye aliingia madarakani kwa mapinduzi ya kijeshi mnamo 2020, walisisitiza umuhimu wa kutatua mzozo wa Niger kwa njia ya amani.

Mali ambayo inapakana na Niger, ilionyesha mshikamano wake na wanajeshi walioshika madaraka mara baada ya mapinduzi ya July 26. **DW**

## Mazungumzo yanahitajika kumaliza mapigano Sudan

**KHARTOUM,** Sudan

NAIBU Mkuu wa Baraza tawala nchini Sudan, Malik Agar amesema kuna ulazima wa kuwa na serikali ya mpito nchini humo kutokana na hali mbaya inayoshuhudiwa kwa sasa.

Agar alisema hayo katika hotuba yake ya moja kwa moja kupitia televisheni na kuongeza kuwa mikakati iliyofanyika ya kuleta amani haikuwa na tija, badala yake njia pekee ya kumaliza mapigano ni mazungumzo.

Mapigano nchini Sudan yanahusisha vikosi vya jeshi la Sudan vinavyoongozwa na Jenerali Abdel Fattah al-Burhan na kikosi cha dharura (RSF) chini ya Jenerali Hamdan Dagalo.

Watu zaidi ya milioni moja wamekimbilia nchi jirani kuomba hifadhi na wengine zaidi ya milioni 3 wakiyakimbia makazi yao kutokana na mapigano yanayoendelea. **DW**

# Wanachama upinzani wakamatwa Zimbabwe

**HARARE,** Zimbabwe

WAKATI joto la uchaguzi linazidi nchini Zimbabwe, polisi wamewakamata wanachama 40 wa chama cha upinzani wakati wakifanya kampeni za lala salama.

Wanachama hao kutoka Chama cha Wananchi na Mabadiliko (CCC), waliokuwa wakifanya kampeni katika kitongoji cha Glenview ambacho kipo katika mji mkuu, Harare.

Uchaguzi wa kumchagua rais na wabunge utafanyika Agosti 23, mwaka huu.

Msemaji wa chama cha CCC, Fadzayi Mahere alichapisha ujumbe katika mtandao wa X, zamani ilijulikana kama Twitter, kuwa mgombea wao Gladmore Hakata, ambaye anagombea ubunge jimbo la glenview Kusini, alikuwa miongoni mwa waliokamatwa.

**CCC ilisema polisi wamepiga marufuku mikutano yake kadhaa tangu tarehe 9 Julai, mwaka huu.**

Hata hivyo, katika taarifa ya polisi iliyosambazwa jana kwenye mitandao ya kijamii, ilisema wanachama wa CCC wanajihusisha na shughuli zisizofaa.

Ilisema, taarifa hiyo kuwa wanachama hao walifanya maandamano ya magari, kuzuia askari wa barabarani kufanya kazi zao na kuimba nyimbo za chama mitaani kitu ambacho kilileta usumbufu kwa wakazi wa eneo hilo.

Kambi ya upinzani mwezi uliopita uliitaka Tume ya Uchaguzi ya Zimbabwe, kuchukua hatua dhidi ya matumizi ya polisi kuvuruga mikutano yao.

CCC ilisema polisi wamepiga marufuku mikutano yake kadhaa tangu tarehe 9 Julai, mwaka huu.

Rais Emmerson Mnangagwa na kiongozi wa CCC Nelson Chamisa, wanachuana vikali katika uchaguzi huo ambao unatarajiwa kuwa wa ushindani. **BBC**



Moto unaendelea kuteketeza nyumba na msitu katika jimbo la Hawaii nchini Marekani kama inavyoonekana katikati ya mji jana. **PICHA: AFP**

# Mwanajeshi Marekani aomba hifadhi nchini Korea Kaskazini

**PYONGYANG,** Korea Kaskazini

SERIKALI ya Korea Kaskazini imesema mwanajeshi wa Marekani, Travis King (pichani) ambaye amekimbilia nchini humo mwezi uliopita, amechukua hatua hiyo kutokana na unyanyasaji na ubaguzi wa rangi ndani ya jeshi la nchi hiyo.

Mwanajeshi huyo Kijana mwenye umri wa miaka 23, alivuka mpaka kutoka Korea Kusini Julai 18, akiwa katika ziara ya kikazi.

Vyombo vya habari vya nchi hiyo vilizema King alienda kutafuta hifadhi Korea Kaskazini.

Hata hivyo, Marekani ilisema haiwezi kuthibitisha madai hayo, ambayo ni maoni ya kwanza kutoka Korea Kaskazini.

Akijibu ripoti za vyombo vya habari vya Korea Kaskazini, afisa mmoja wa Pentagon alisema kipaumbele chao ni kuwa King arudishwe nyumbani salama kupitia njia zote zinazofaa,

Awali mamlaka zilisema zinaamini kuwa mwanajeshi huyo alivuka mpaka makusudi.

Tangu wakati huo, hakuwahi kuonekana tena, lakini ripoti ya shirika la habari la serikali ya Korea Kaskazini (KCNA) ilisema mwanajeshi huyo amekiri kuingia kwa makusudi eneo la Korea Kaskazini kinyume cha sheria, lakini hakusema iwapo atakabiliwa na mashtaka au adhabu nyingine.

Travis King ni mtaalamu wa upelelezi ambaye amekuwa jeshini tangu Januari 2021 na alikuwa Korea Kusini kama sehemu ya zamu ya majukumu yake.

Kabla ya kuvuka mpaka, alitumikia kifungo cha miezi miwili nchini Korea Kusini kwa mashtaka ya shambulio na aliachiliwa julai 10.

Alitakiwa kurejea Marekani kwa ajili ya kukabiliwa na kesi nyingine za kinidhamu, lakini alitoroka uwanja wa ndege na kwenda eneo la mpaka linaloitwa Demilitarized Zone (DMZ), ambalo linatenganisha Korea Kaskazini na Kusini.

"Wakati wa uchunguzi, Travis King alikiri kwamba aliamua kuja Korea Kaskazini kwa kuwa alikuwa na hisia mbaya dhidi ya unyanyasaji wa kinyama na ubaguzi wa rangi ndani ya Jeshi la Marekani," KCNA ilisema.

Iliongeza taarifa hiyo "Pia alionyesha nia yake ya kutafuta hifadhi ya ukimbizi katika Korea Kaskazini au nchi ya tatu, akisema kuwa amekatishwa tamaa na jamii isiyo sawa ya Marekani."




Familia Travis King, katika mahojiano na ABC News mapema mwezi huu, ilisema aliwaambia alikabiliwa na tatizo la ubaguzi wa rangi jeshini.

Pia walisema afya yake ya akili ilionekana kutokuwa sawa kabla ya kutoweka. **BBC**

MWAMUZI MKONGWE HAMDUNI:

# Marefa wa Tanzania ni bora zaidi wanapokuwa nje, shida nyumbani

INATOKA UKURASA 24

kinyume chake kupwaya katika mechi za nyumbani. Kutokana na hali hiyo, mkongwe huyo anawasilisha wazo lake la kitaalamu, haja ya kuwapo mitambo ya VAR, akiamini ina nafasi kubwa ya kuziba pengo linaloshuhudiwa.

Vilevile, anawatetea waamuzi dhidi ya malalamiko ya mashabiki kwamba kupitia televisheni wana fursa ya kuchambua makosa kwa sababu yanarudiwa, huku mwamuzi akibakiwa na upeo pekee wa kile alichokiona mara moja.

“Sisi tupo chini ya TFF. Endapo (shirikisho) litafikia hatua hiyo, sisi tutaliunga mkono. Hatuna tatizo kuletewa VAR kwa sababu tutapunguza makosa,” anatamka Hamduni, huku akifafanua uhalisia wa soka duniani sasa linachezwa kwa kasi, hivyo hitaji la VAR haliepukiki kupata usahihi.

Anaendelea kwa mifano: “Ukiona malalamiko mengi, yote yanakuja kwa sababu ya kuona marudio, ndiyo zinalalamikiwa dosari ndogondogo.

“Kwangu ninaunga mkono na ninawaomba sana wadau wa michezo wanaosimamia mashindano vitu kama hivyo vinapatikana watusaidie ili tuondokane na hili jambo. Ukweli linatukwaza sana na sisi hatupendi.”

Katika maoni yake kuhusu haja ya kuleta waamuzi wa kigeni kusimamia mechi zenye upinzani, hususani za Simba dhidi ya Yanga, hakubaliani nayo, akiamini hadi sasa Tanzania ina waamuzi bora wa kuhimili mvutano huo.

“Hilo suala ni zuri, lakini linachukuliwa na TFF na kanuni zake za ligi. Sisi tunapenda ushirikiano na waamuzi kutoka nje kwa sababu na sisi tutajifunza mawili matatu kutoka kwao.

“Lakini ninataka kuwaeleza watu, wadau wote kuwa, suala la malalamiko utamwangalia mtu analalamika, lakini ukimwuliza analalamikia nini, hakuelezi.

“Kikubwa katika hili jambo ni lazima tusimamie sheria 17 za soka, lakini ninataka kueleza wazi kwanza tuendelee kuwaamini waamuzi wetu, isipokuwa mihemko hasa ya ‘dabi’ imekuwa mikubwa sana.

“Hatuwezi kuizuia kwa sababu kila mmoja anahitaji matokeo na hasa timu inaposajili vizuri na upenzi na mnafahamu kwamba, ligi yetu kwa sasa imekuwa bora na ngumu sana. Inakamata nafasi ya tano kwa ubora Afrika...

“Tunaona jinsi serikali na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ilivyowekeza kwenye michezo na kuipaisha kimataifa. Rais wa TFF, Wallace Karia anavyohangaika kutafuta wahisani wa wadau kwa ajili ya kuwekeza kwenye soka.

“Tunawapongeza kwa hilo, na hili linaleta msisimko mkubwa kiasi kila timu kuhitaji matokeo. Hakuna anayekubali kushindwa kirahisi, mpaka kuweza hata kulalamikia vitu vidogo vidogo vya kibinadamu vya waamuzi ambavyo vinatokea dunia nzima,” anafafanua.

**WAENDAKO**

Hamduni anasema azma ni kuendelea kukaa na waamuzi kuelekezana, kuwafundisha na kuwapa adhabu pale watakapofanya vibaya katika Ligi Kuu msimu ulioanza.

“Tunawahakikisha tutajitahidi sana na tumekuwa tunajitahidi, mmekuwa mashuhuda wa Ligi Kuu msimu uliopita, japo kulikuwa na dosari chache, lakini wadau wote walitupongeza.

“Watanzania tuwe na tabia ya kuaminiana kwa sababu tukianza kusema waamuzi watoke nje, basi kila kitu tutataka kitoke nje - walimu, madereva nao watoke nje, kifupi tuaminiane!” anasisitiza.

Huku akirejea waamuzi wakongwe wa Zanzibar kama Hafidh Ally na Juma Ali David waliokuwa wanaalikwa kuchezesha Ligi Kuu Tanzania Bara, bado anatetea kutokuwapo wenza hao wa visiwani hakujaipa pengo la uamuzi katika ligi hiyo.

“Kwa sasa kanuni zetu zinatuelekeza hivyo. Bara tuna waamuzi wengi na wanajitosheleza. Tuna ushirikiano pale mashindano yanapokuwa ni ya Muungano. Kwahiyo, hatushirikiani nao kwenye Ligi Kuu mpaka hapo kanuni zitakapobadilishwa,” anahitimisha kiongozi huyo wa waamuzi.

***USIKOSE KESHO NENO LAKE KUHUSU MAISHA YA KIINACHOENDELEA UWANJANI***



Mshambuliaji wa Geita Gold FC, Elias Maguli akimiliki mpira wakati wa mchezo wao wa ligi kuu dhidi ya Ihefu FC kwenye uwanja wa Highlanders, Mkoani Mbeya, Geita ilishinda bao 1-0, bao lilitoka kwa Maguli. **PICHA:MTANDAO**

# Bingwa duniani kusaidia mabondia wazawa

**Na Saada Akida**

BONDIA wa kimataifa wa Uingereza anayeshikilia taji la Dunia uzito wa ‘Light Middle’ Natasha Jonas, amesema atakaporejea kwao atazungumza na wanaomsimamia kwa ajili ya kuona jinsi ya kufikia malengo ya kuunyanyua mchezo wa ngumi hapa nchini.

Bondia huyo yupo hapa nchini kwa ajili ya mapumziko mafupi na kutembelea mikoa mbalimbali ikiwemo Arusha, Zanzibar na Dar es Salaam pamoja na kuzungumza na mabondia mbalimbali katika mikoa hiyo.

Akizungumza na Nipashe jana, Natasha alisema baada ya kutembelea ameona changamoto za mabondia na anatarajia atakaporejea Uingereza atakutana na wasimamizi wake kwa ajili ya kuona jinsi gani wanaweza kunyanyua mchezo wa ngumi hapa nchini na kuwasaidia mabondia.

“Natamani zaidi kuona mchezo wa ngumi hapa Tanzania unakuja juu baada ya kuona baadhi ya mabondia kuwa na vipaji vikubwa, nimemuona bondia kama Hassan Mwakinyo ana kipaji sana, na yeye amenishawishi sana kuja kufanya mapumziko yangu huku Tanzania, nimefanikiwa kutembelea baadhi ya sehemu wanazofanyia mazoezi na kuona changamoto za vifaa vya mazoezi kwa mabondia,” alisema Jonas.

Alisema akirejea Uingereza atakutana na watu wake na kuweka mipango ya kuona namna gani wanawasaidia mabondia wa Tanzania.

Natasha aliongezea kusema “Natamani zaidi kuona mabondia wanawake wanafanya vizuri hasa katika mapambano ya kimataifa ili kujitangaza zaidi kwa kupata nafasi kama ilivyo kwake, tutaona namna gani tunaweza kusaidia,” alisema Jonas.

## Dabo awatoa hofu mashabiki wa Azam FC

**Na Mwandishi Wetu,** TANGA

KOCHA Mkuu wa Azam FC, Yousouph Dabo, amesema bado ana muda wa kukijenga kikosi chake na anaamini kitafanya vizuri katika mechi za Ligi Kuu Bara na mashindano ya kimataifa watakayoshiriki.

Baada ya kichapo cha mabao 2-0 kutoka kwa Yanga, Azam sasa inasubiri kucheza mechi ya kuwania mshindi wa tatu.

Dabo aliliambia gazeti hili matokeo ya mchezo huo wa juzi yamewaumiza lakini yamempa nafasi ya kubaini mapungufu na kuanza kuyafanyia kazi.

“Bado nina muda wa kurekebisha mambo, tumecheza mchezo mgumu dhidi ya Yanga na nimeona nini kinatakiwa kuongezwa katika kikosi changu, tumepoteza kwa sababu wenzetu Yanga walikuwa na wakati mzuri, nitazitumia vizuri siku zilizobaki kuakikisha tunakuwa sawa kuelekea kwenye ligi,” alisema Dabo.

Licha ya kuanza kupoteza taji la kwanza, kocha huyo alisema bado mipango yake msimu huu ni kufanya vizuri zaidi ya msimu uliopita.

## Maxime: Tumejipanga kutoa dozi 2023/2024

**Na Adam Fungamwango**

ZIKIWA zimebakia siku chache kabla ya kuanza kwa msimu mpya, Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Mecky Maxime, amesema anaamini atafanya vyema katika Ligi Kuu Tanzania Bara kutokana na usajili mzuri waliofanya.

Akizungumza mara baada ya kuwasili kutoka Uganda walipokwenda kucheza mechi za kirafiki, Maxime alisema namna kikosi chake kilivyoimarika, anaamini atatetemesha kila timu watakayokutana nayo.

“Usajili ulienda vizuri na tumeshamaliza mambo hayo na tukaanza ‘pre season’, sasa tuna mwendelezo mzuri tu, na tupo tayari kwa ligi, unajua katika soka usiangalie sana usajili wa wenzako, angalia wewe mwenyewe umejipanga vipi kukabiliana na yoyote atakayekuja,” alisema Maxime.

Aliongeza mechi nne za kirafiki walizocheza zimempa mwanga wa kikosi chake na hakuzingatia matokeo waliyopata.

“Tumecheza mechi nne za kirafiki, kwetu kipimo hicho kilikuwa kizuri sana kwa sababu ukipata timu za Kiganda ziko vizuri zinakusaidia kufahamu ubora wako,” Maxime alisema.

## ZISIKUPITE

### AMRABAT ANUKIA MAN

KLABU ya Manchester United ipo katika harakati za mwisho kutoa ofa rasmi kwa kiungo wa Fiorentina na Morocco, Sofyan Amrabat, 26. ***(La Nazione)***

### BECKER HANA MPANGO

MCHEZAJI wa kimataifa wa Brazil, Alisson Becker hana mpango wa kuondoka Liverpool na ana furaha kuwa kipa namba moja wa kocha Jurgen Klopp. ***(Anfield Watch)***

### AL-NASSR WAMTAKA

TIMU ya Saudi Arabia Al-Nassr ilisemekana kutaka kumsajili Alisson Becker, 30, na kwamba alikuwa na nia ya kuihama klabu hiyo. ***(Footmercato)***

### MO SALAH NAYE

MSHAMBULIAJI wa Misri, Mohamed Salah, 31, ameripotiwa "kuitaka" timu moja ya Saudi Pro League kufanya mazungumzo na Liverpool kuhusu uwezekano wa uhamisho msimu huu. ***(Alkass, kupitia Football365)***

### ONANA BADO WA EVERTON

KLABU ya Everton haijapokea ofa kutoka kwa Manchester United kuhusu kiungo wa Ubelgiji, Amadou Onana, 21, na ni ada kubwa tu ya uhamisho itakayomuwezesha kuondoka pale Goodison Park. ***(Liverpool Echo)***

### CITY WAKOMAA NA PAQUETA

KLABU ya Manchester City inatazamiwa kuwasilisha ombi jipya la kumnunua kiungo wa kati wa West Ham na Brazil, Lucas Paqueta, 25, katika saa 24 zijazo. ***(Football Insider)***

### OLISE AKARIBIA CHELSEA

KLABU ya Crystal Palace inaamini kuwa Chelsea imevuka mipaka katika mwenendo wao wakati wa kujaribu kumsajili winga wa Ufaransa chini ya umri wa miaka 21, Michael Olise, 21. ***(Mail)***

### LLORIS ATAKIWA LAZIO

LAZIO imeanza mazungumzo na mlinda mlango wa Tottenham Hotspur na Ufaransa, Hugo Lloris, 36, kuhusu uwezekano wa kuhamia Ligi Kuu Italia. ***(Gianluca di Marzio)***

### ATAKIWA SAUDI ARABIA

KLABU ya Fulham imepokea ofa ya karibu pauni milioni 47 kutoka kwa Al-Hilal kwa mshambuliaji wa Serbia, Aleksandar Mitrovic, 28, huku mchezaji huyo akitaka kuhamia klabu hiyo ya Saudi Arabia. ***(TalkSport)***

### PALHINHA ALENGWA

LIVERPOOL inafikiria kuwalenga wachezaji sita wa safu ya kati, akiwemo mchezaji wa Fulham na Ureno, Joao Palhinha, 28 na kiungo wa kati wa Crystal Palace na Mali, Cheick Doucoure, 23. ***(Mail)***

### BARCO AIVUTIA BRIGHTON

KLABU ya Brighton inavutiwa na beki wa kushoto wa Boca Juniors, Valentin Barco, 19, huku Muargentina huyo akisemekana kuwa na kipengele cha kuachiwa cha takribani pauni milioni 8. ***(Brighton Argus)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# DILI LA MAGUIRE KWENDA WEST HAM LAKWAMA

**MANCHESTER,** England

● ● ● Mshahara wa Muingereza huyo watajwa kuwa sababu ya kukosa timu, United sasa...

UHAMISHO uliopendekezwa wa Harry Maguire kwenda West Ham United umeshindikana, kwa mujibu wa 90min.

**Baada ya kumwambia Maguire kuwa yuko huru kuondoka Old Trafford msimu huu wa joto, Manchester United awali ilikataa dau la pauni milioni 30 kutoka kwa West Ham huku kukiwa na wasiwasi juu ya uwezo wao wa kukidhi matakwa ya mshahara wa beki huyo wa kati.**

West Ham wamekamilisha usajili wa Edson Alvarez na James Ward-Prowse, lakini mazungumzo kuhusu Maguire yaliendelea kusuasua huku wakishindwa kufikia makubaliano kuhusu mshahara na beki huyo.

Maguire alikuwa amekubaliana maslahi binafsi kwa mshahara uliopunguzwa na West Ham, lakini akataka kiwango kingine kilipwe na United ili kufidia hasara kwa kipindi cha miaka miwili iliyobaki ya mkataba wake na klabu hiyo ya Old Trafford.

Vyanzo vya habari sasa vimethibitisha kuwa hakuna makubaliano yaliyofikiwa kati ya Maguire na United, na kuwalazimu West Ham kukubali kushindwa katika harakati zao za kumnasa beki huyo.

United walikuwa wakijiandaa kuondoka kwa Maguire kwa kuzungumza na Bayern Munich kuhusu beki Mfaransa Benjamin Pavard, lakini sasa Mashetani Wekundu hao wanahofia hawana nafasi ya kifedha ya kusajili beki mwingine huku mshahara mkubwa ya Maguire ukiwa bado upo.

Man United sasa haitarajii ofa kutoka Klabu nyingine kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, ambaye anaonekana atabakia Old Trafford zaidi ya msimu huu wa joto.

Kocha Erik ten Hag anajulikana kuwa na furaha kuendelea kufanya kazi na Maguire kama mbadala wa Raphael Varane na Lisandro Martinez, lakini hivi majuzi alimuonya mchezaji huyo wa kimataifa wa England kwamba yuko kwenye vita ya kuwania dakika kama ataamua kubaki.

Maguire bado ana mkataba na United hadi mwaka 2025, huku akiwa na kipengele cha kuongeza miezi 12.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,144,17
MECHI KALI
MTIBWA SUGAR
VERSUS
SIMBA SC
1 | 7.50
X | 3.20
2 | 1.45
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# LIONEL MESSI MECHI SITA, MABAO TISA

**MIAMI,** Marekani

MICHEZO sita, mabao tisa, mechi moja ya fainali kwa Lionel Messi baada ya Jumanne usiku kufunga kwenye ushindi wa 4-1 wa Inter Miami CF dhidi ya Philadelphia Union katika nusu fainali ya Kombe la Ligi Uwanja wa Subaru Park huko Chester, Pennsylvania.

Mabao ya kipindi cha kwanza kutoka kwa Messi, Josef Martínez na Jordi Alba yaliifanya Miami kupata uongozi usioweza kushindwa na kuiwezesha kutinga fainali ya kwanza ya Kombe la Ligi, na kushinda kila mechi tangu bingwa huyo wa Kombe la Dunia na Argentina alipojiunga na klabu hiyo Julai.

Timu hiyo inayonolewa na kocha Gerardo Martino itacheza na Nashville SC iliyoshinda 2-0 dhidi a Liga MX Monterrey katika nusu nyingine. Sasa timu hizo zitacheza fainali Jumamosi kule Nashville.

Miami pia ilifanikiwa kutinga fainali ya Kombe la Mabingwa la Concacaf 2024 -- la kwanza katika historia ya timu hiyo -- kwa kufika fainali.

"Timu imefika fainali ya mashindano ya kimataifa," alisema Martino.

"Moja ya malengo ni kufuzu kwa Kombe la Mabingwa wa Concacaf, sasa tunatakiwa kujiandaa kujaribu kutwaa ubingwa ikiwezekana, tuna ari na kujiamini, lakini pia tumejikita katika kufanya kila kitu ili kujiweka vizuri zaidi, tunataka kuifanya klabu hii kuwa ya ushindi."



## De Bruyne nje ya dimba miezi 4

**MANCHESTER,** England

KIUNGO wa kati wa Manchester City, Kevin De Bruyne anaweza kukosa kwa kipindi cha miezi minne ijayo huku klabu ikipanga kuamua iwapo mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji anahitaji kufanyiwa upasuaji wa jeraha la misuli ya paja, kocha Pep Guardiola amesema.

De Bruyne alichechemea katika kipindi cha kwanza cha ushindi wa 3-0 wa City dhidi ya Burnley Ijumaa baada ya kujirudia kwa tatizo hilo ambalo lilikatiza ushiriki wake katika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya Juni.

Akizungumza kabla ya mechi ya timu yake ya Super Cup dhidi ya Sevilla mjini Athens jana, Guardiola aliwaambia waandishi wa habari: "Ni jeraha baya.

"Tunapaswa kuamua kama anahitaji upasuaji au hakuna upasuaji lakini atakuwa nje kwa miezi michache. Uamuzi wa upasuaji utachukuliwa katika siku chache zijazo. Itakuwa kati ya miezi mitatu au minne."

De Bruyne alikosa mechi za City kabla ya msimu mpya lakini akarejea katika kipindi cha pili cha kwenye mchezo wa Ngao ya Jamii walipofungwa na Arsenal.



72,464/-

# KAZE ALIA NA LUSAJO KIPIGO CHA NAMUNGO NYUMBANI

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Namungo FC, Cedric Kaze amesema kukosekana kwa mshambuliaji wake tegemeo, Reliants Lusajo ni moja ya sababu iliyosababisha kipigo cha bao 1-0 juzi nyumbani, dhidi ya timu iliyopanda daraja msimu huu ya JKT Tanzania.

Kaze, kocha msaidizi wa zamani wa Yanga, ameanza vibaya kwenye timu yake mpya hiyo akiwa kocha mkuu baada ya kuchapwa kwenye mechi ya kwanza, ikiwa ni mara ya kwanza kwa timu hiyo tangu ilipoanza kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2019/20.

"Mpira ndivyo ulivyo aliyecheza vizuri anaweza kufungwa, wenzetu wamefanya mashambulizi machache tu lakini wamepata bao na baada ya hapo wakaja na mkakati wa kulilinda, wakati mwingine ni bahati, sisi tumegongesha mwamba mara mbili, naamini bahati tu haikuwa upande wetu, pia hatukuwa na straika halisi wa kati kwenye kikosi chetu kwani Lusajo bado anaumwa na Kelvin Sabato tuliyemsajili msimu huu hajakuwa kwenye utimamu wa mwili kuweza kucheza, naamini kama tungekuwa na straika halisi kama Lusajo nadhani hadithi ingekuwa nyingine," alisema Kaze.

Msimu uliopita kwenye mechi ya kwanza ya ligi Namungo ikicheza Uwanja wa Banjamin Mkapa, Dar es Salaam, uwanja wao ukiwa kwenye matengenezo ilitoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Mtibwa Sugar, mabao yote mawili yakifungwa na Lusajo, na msimu 2021/22 iliichapa Geita Gold mabao 2-0, Uwanja wa Majaliwa, moja likiwekwa na Lusajo.

Msimu wa kwanza ikicheza Ligi Kuu 2019/20, Namungo ilipata ushindi mechi ya kwanza nyumbani wa mabao 2-1 dhidi ya Ndanda FC, na uliofuata, 2020/21 iliidungua Coastal Union bao 1-0.

Kwa msimu mitano sasa Namungo haijawahi kucheza mechi ya ufunguzi ugenini, badala yake inacheza nyumbani, ikishinda mechi tatu, sare moja na ikipoteza moja.

Kocha Mkuu wa JKT Tanzania, Malale Hamsini aliwapongeza wachezaji wake kwa kujituma na kusema ilikuwa mechi ngumu ambayo walicheza kimkakati zaidi.

"Niliwaambia wachezaji wangu wasitokae sana nyuma kwa sababu tayari tuna mtaji wa bao moja na kweli Mungu amesaidia tumeshinda," alisema.



Wanamuziki wa Bendi ya muziki ya Tanzanite, wakitumbuiza katika uzinduzi wa nembo ya ubora ya mfumo dhamana wa bidhaa za Kampuni ya Alaf uliofanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Gamondi awaongezea dozi wachezaji

INATOKA UKURASA 24

Gamondi.

Kocha huyo alisema amekaa na wachezaji wake na ameapa maelekezo ambayo kama watayafanyia ana uhakika wakufanya vizuri kwenye ligi na mashindano ya kimataifa.

Wachezaji wa Yanga kwa sasa wanafanya mazoezi wakitokea nyumbani na kesho Ijumaa wataingia kambini tayari kujiandaa na mchezo huo dhidi ya ASAS.

## *Kocha Robertinho ataka 'kishindo'*

INATOKA UKURASA 24

ho.

Kwa upande wake, Kocha wa Mtibwa Sugar, Habib Kondo alisema wapo tayari kukabiliana na Simba.

Alisema wamefanya maandalizi ya kutosha na wanafahamu ubora wa wapinzani wao hao.

"Kama timu tupo tayari, tunajua mchezo hautakuwa mwepesi lakini lazima tutumie faida ya kucheza uwanja wa nyumbani, wachezaji wangu wameonyesha kuitaka hii mechi, tusubiri baada ya dakika 90 alisema Kondo.

## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 19/08/23 | 17:00 | Fulham FC vs Brentford FC | 2.55 | 3.25 | 2.60 |
| 02. 19/08/23 | 19:15 | Caykur Rizespor vs Alanyaspor | 2.36 | 3.25 | 2.55 |
| 03. 19/08/23 | 19:30 | Tottenham Hotspur vs Manchester United | 3.00 | 3.40 | 2.21 |
| 04. 19/08/23 | 19:30 | Empoli FC vs Hellas Verona | 2.35 | 3.15 | 2.95 |
| 05. 19/08/23 | 21:45 | Hatayspor Antakya vs Kasimpasa Istanbul | 2.32 | 3.35 | 2.60 |
| 06. 19/08/23 | 21:45 | Genoa CFC vs ACF Fiorentina | 2.95 | 3.25 | 2.30 |
| 07. 19/08/23 | 22:30 | Portimonense SC vs Boavista Porto | 2.43 | 3.10 | 2.90 |
| 08. 19/08/23 | 22:30 | CA Osasuna vs Athletic Bilbao | 2.75 | 3.05 | 2.60 |
| 09. 20/08/23 | 14:30 | VfL 1899 Osnabruck vs FC Nuremberg | 2.48 | 3.40 | 2.60 |
| 10. 20/08/23 | 14:30 | Holstein Kiel vs FC Magdeburg | 2.35 | 3.55 | 2.70 |
| 11. 20/08/23 | 16:00 | Le Havre AC vs Stade Brest 29 | 2.55 | 3.20 | 2.65 |
| 12. 20/08/23 | 16:00 | FC Lorient vs OGC Nice | 3.05 | 3.40 | 2.18 |
| 13. 20/08/23 | 17:30 | Estoril Praia vs Rio Ave FC | 2.40 | 3.15 | 2.90 |
| 14. 20/08/23 | 18:00 | Hamarkameratene vs Rosenborg BK | 2.70 | 3.25 | 2.26 |
| 15. 20/08/23 | 19:00 | FC Sudtirol Bolzano vs Spezia Calcio | 3.15 | 2.95 | 2.15 |
| 16. 20/08/23 | 20:15 | KV Kortrijk vs KAS Eupen | 2.15 | 3.45 | 3.10 |
| 17. 20/08/23 | 21:45 | RC Lens vs Stade Rennes | 2.33 | 3.50 | 2.75 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### ALHAMISI - 17/08/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 12:00 | 4078 | Bayern Munich U19 vs FC Augsburg U19 | 1.54 | 4.29 | 4.59 |
| 16:00 | 5284 | Mtibwa Sugar vs Simba | 7.50 | 3.20 | 1.45 |
| 18:00 | 4732 | Dhamk vs AL Riyadh | 1.93 | 3.36 | 3.93 |
| 18:30 | 5494 | Qatar SC vs Al Gharafa SC | 2.25 | 3.28 | 2.77 |
| 19:00 | 1087 | Lincoln FC vs KF Ballkani | 4.29 | 3.69 | 1.74 |
| 19:00 | 1220 | Esteghlal Tehran vs Malavan Bandar Anzali | 1.55 | 3.75 | 5.28 |
| 19:00 | 2212 | Pyunik Yerevan vs Bodo Glimt | 4.30 | 3.80 | 1.71 |
| 19:00 | 2270 | Aktobe vs Sepsi Osk | 2.76 | 3.06 | 2.56 |
| 19:00 | 4113 | Pogon Szczecin vs KAA Gent | 3.25 | 3.60 | 2.02 |
| 19:00 | 5644 | HJK Helsinki vs Karabakh | 2.55 | 3.46 | 2.50 |
| 19:00 | 5911 | Al Ahli Amman vs Sahab Club | 2.86 | 3.12 | 2.33 |
| 20:00 | 1069 | Besiktas vs Neftchi Baku | 1.18 | 6.40 | 13.01 |
| 20:00 | 1734 | Apoel Nicosia vs Dila Gori | 1.39 | 4.29 | 7.98 |
| 20:00 | 3132 | Brann vs FC Arouca | 2.08 | 3.44 | 3.24 |
| 20:00 | 3448 | Gzira United vs Viktoria Plzen | 6.42 | 4.61 | 1.41 |
| 20:00 | 3590 | IFK Luleaa vs Notvikens IK | 1.05 | 10.21 | 19.41 |
| 20:00 | 3718 | Austria Vienna vs Legia Warszawa | 2.55 | 3.46 | 2.50 |
| 20:00 | 4400 | Nordsjalland vs Steaua Bucuresti | 1.68 | 3.60 | 4.81 |
| 20:00 | 4964 | Dynamo Kiev vs Aris Salonica | 1.66 | 3.65 | 4.90 |
| 20:00 | 5219 | Levski Sofia vs Hapoel Beer Sheva | 2.36 | 3.10 | 3.00 |
| 20:00 | 5340 | Ferencvaros TC vs Hamrun Spartans | 1.14 | 7.43 | 14.05 |
| 20:00 | 5348 | Maccabi Tel Aviv vs AEK Larnaca | 1.56 | 3.79 | 5.78 |
| 20:00 | 5450 | Skellefteaa FF vs Storfors Aik | 1.05 | 9.98 | 21.39 |
| 20:00 | 5603 | BK Hacken vs Zalgiris | 1.52 | 4.12 | 5.62 |
| 20:00 | 5858 | FC Riga vs Twente | 3.99 | 3.84 | 1.76 |
| 20:30 | 1610 | AL Markhiya vs Al Rayyan SC | 4.05 | 3.79 | 1.67 |
| 20:30 | 4353 | Breidablik vs Zrinjski Mostar | 2.50 | 3.46 | 2.55 |
| 20:45 | 3262 | Midtjylland vs Omonia Nicosia | 1.47 | 4.18 | 6.17 |
| 21:00 | 1323 | Neman Grodno vs NK Celje | 2.70 | 3.25 | 2.49 |
| 21:00 | 1541 | Partizani Tirana vs Valmiera Fk/Bjss | 1.46 | 4.30 | 6.19 |
| 21:00 | 2244 | Al Khaleej Club vs Al Ahli Jeddah | 2.99 | 3.20 | 2.37 |
| 21:00 | 2552 | NK Osijek vs Adana Demirspor | 2.60 | 3.30 | 2.55 |
| 21:00 | 2800 | BATE Borisov vs Sheriff Tiraspol | 2.80 | 3.55 | 2.26 |
| 21:00 | 2831 | Grindavik W vs Grotta W | 3.06 | 3.83 | 1.95 |
| 21:00 | 3614 | Spartak Trnava vs Lech Poznan | 2.99 | 3.39 | 2.22 |
| 21:00 | 3761 | Ludogorets Razgrad vs Astana | 1.48 | 4.10 | 6.21 |
| 21:00 | 3797 | Swift Hesperange vs FC Struga Trim Lum | 1.71 | 3.71 | 4.41 |
| 21:00 | 4017 | KR Reykjavik W vs HK Kopavogur W | 9.18 | 6.53 | 1.19 |
| 21:00 | 5005 | Atletico Grau vs Sporting Cristal | 3.33 | 3.07 | 2.07 |
| 21:00 | 5096 | KA Akureyri vs Brugge | 12.00 | 6.40 | 1.19 |
| 21:15 | 3241 | Maribor vs Fenerbahce | 4.60 | 3.90 | 1.65 |
| 21:15 | 4888 | HNK Rijeka vs B36 Torshavn | 1.21 | 6.19 | 10.99 |
| 21:30 | 2897 | Al-Jalil vs AL Aqaba | 2.58 | 2.88 | 2.73 |
| 21:45 | 1116 | Hearts vs Rosenborg | 2.21 | 3.40 | 3.00 |
| 21:45 | 4748 | FC Luzern vs Hibernian | 1.76 | 3.71 | 4.11 |
| 22:00 | 1832 | Debreceni VSC vs Rapid Vienna | 2.69 | 3.19 | 2.54 |
| 22:00 | 3770 | Libertad Loja vs Delfin SC | 2.70 | 3.21 | 2.39 |
| 22:00 | 4125 | Partizan vs Sabah | 1.66 | 3.84 | 4.58 |
| 22:15 | 1581 | Afturelding Mosfellsbaer W vs Vikingur Reykjavik W | 4.20 | 4.20 | 1.55 |
| 22:15 | 5584 | Fylkir Reykjavik W vs Augnablik W | 1.06 | 8.40 | 17.00 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Alhamisi Agosti 17, 2023

Nipashe




Dili la Maguire lakwama

UKURASA 21

# Kocha Robertinho ataka 'kishindo' akianza ligi leo

## ●●● Asema ushindi Ngao ya Jamii umewaongezea hamasa wachezaji

**Na Adam Fungamwangwo**

KOCHA wa Simba, Roberto Oliviera 'Robertinho' amesema anataka kuanza kwa kishindo ligi kuu leo atakapowakaribisha Mtibwa Sugar kwenye uwanja wa Manungu.

**Wakati Robertinho akijinasibu hivyo, Simba ina rekodi ya kutokufungwa katika mchezo wa kwanza wa kuanza kwa msimu katika miaka 16.**

Simba ilipoteza mchezo wa kwanza wa ufunguzi wa ligi mwaka 2007 ilipokubali kipigo cha bao 1-0 kutoka kwa Coastal Union kwenye Uwanja wa Mkwakwani, bao likifungwa na Sunday Peter katika dakika ya 44 ya mchezo.

Tangu hapo Simba haijapoteza mchezo wowote wa kwanza wa ligi na leo itakuwa na kibarua mbele ya Mtibwa Sugar.

Kocha Robertinho amesema wanataka kuanza kwa kishindo kwenye mchezo huo waleo na kuwataka wachezaji wake kusahahu ushindi wao wa penalti wa Ngao ya Jamii jumapili iliyopita dhidi ya Yanga.

" Nataka kuanza vizuri, nimewaambia wachezaji wangu tupambane kwa ajili ya pointi tatu, unaponza kwa ushindi unazidisha morali kwenye timu, nafahamu mchezo hautakuwa mwepesi kwa sababu na wapinzani wetu wamejiandaa kushinda, lakini kama Simba ni lazima tuonyeshe ukubwa wetu," alisema Robertinho.

"Tumejiandaa vyema na mchezo huu, wachezaji wetu wako fiti tunatarajia tutacheza vizuri, kwa nidhamu na ubora ili kupata ushindi," alisema.

Kikosi cha Simba kitaingia uwanjani kikiwa na kazi moja tu ya kuwathibitishia wanachama na mashabiki wa timu hiyo kuwa hawakubahatisha kutwaa Ngao ya Jamii hivyo kusaka ushindi kwa udi na uvumba, ikiwa pia kuendelea na kampeni yao ya kukusanya vikombe msimu huu.

Itakuwa ni mechi ya tatu kwa timu hizo kukutana kwenye Uwanja wa Manungu tangu ufunguliwe, na miwili ya mwanzo iliyochezwa, Simba ilishinda mmoja na mwingine zikitoka suluhu.

Msimu wa 2021/22 zilitoka suluhu kwenye uwanja huo na msimu uliopita Simba ilishinda mabao 3-0 yaliyofungwa na Jean Baleke ambaye yupo kwenye kikosi na huenda akacheza kwenye pambano la leo.

Kocha Robertinho aliweka wazi kuwa wataendelea kumkosa beki wao wa kati Henock Inonga ambaye aliumia bega kwenye mchezo wa nusu fainali ya Ngao ya Jamii dhidi ya Singida Fountaine Gate.

"Inonga atakuwa nje ya uwanja kwa wiki mbili, utakumbuka aliumia bega tukiwa Tanga na amerejea Dar es Salaam, lakini taarifa njema ni kwamba tuna kipa wetu mpya Lakred ambaye ameshawasili huku kutoka Morocco," alisema Robertin-

INAENDELEA UKURASA 23

# Gamondi awaongezea dozi wachezaji

**Na Saada Akida**

KUELEKEA kwenye mchezo wao wa kwanza hatua ya awali ya ligi ya mabingwa Afrika dhidi ya ASAS ya Djibouti, Kocha wa Yanga Miguel Gamondi amewaongezea dozi ya mazoezi wachezaji wake.

Gamondi juzi alibadili mazoezi ya timu asubuhi kwa kuwapeleka wachezaji 'Gym' na baadae jioni wakafanya mazoezi ya uwanjani.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Gamondi alisema ameongeza dozi ya mazoezi kwa kuwa kuna kitu kiufundi amekiona na ameamua kukifanyia kazi ili kupata ushindi kwenye mchezo wa Jumapili.



"Tunataka ushindi, nataka kila mchezaji awe fiti kimwili, tutakuwa tukifanya mazoezi mara mbili kwa siku kadhaa tukianzia Gym, kikubwa tunataka ushindi," alisema Gamondi.

Alisema kwenye mazoezi ya uwanjani, anaifanyia kazi safu yake ya ushambuliaji kwa kuiongezea makali.

"Tunaanza na Asas FC, tunahitaji matokeo mazuri kujiweka katika mazingira mazuri ya kuendelea hatua inayofuata, wachezaji wako vizuri na katika mazingira mazuri ya kushindana sina wasiwasi na wao kwenye hilo, lakini tunarekebishana zaidi katika nafasi za mbele," alisema kocha huyo.

Alisema ana washambuliaji wazuri na wenye uwezo mkubwa lakini kuna dosari kidogo ameziona na lazima afanyie kazi.

"Katika mchezo uliopita dhidi ya Simba tulitengeneza nafasi nyingi lakini hatukuzifanyia kazi, lazima niweke mambo sawa kwa sababu kuna michezo mingi mbele yetu lazima tuwe vizuri kila idara," alisema

INAENDELEA UKURASA 23

MWAMUZI MKONGWE:

# Marefa wa Tanzania ni bora zaidi wanapokuwa nje, shida nyumbani

**Na Adam Fungamwangwo**

MWENYEKITI wa Kamati ya Waamuzi ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Nassor Hamduni amesema Tanzania ina waamuzi bora zaidi kwa Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), lakini wanapokuwa nyumbani wanapwaya.

Hamduni ambaye ni mkongwe wa kimataifa katika fani hiyo nchini, anaieleza Nipashe katika mazungumzo maalum kwamba: "Huko nje wanafanya vyema sana, tatizo linakuja wakichezesha hapa (nyumbani), kunakuwa na presha nyingi kwa sababu hatakiwi na mashabiki kufanya kosa hata la kibindamu wakati hakuna VAR."

Mwanataaluma huyo anafafanua kuwa ubora wa waamuzi hao, akitumia ushahidi linganifu kwamba wanatia fora wanapokuwa ugenini kuchezesha, lakini

INAENDELEA UKURASA 20




Mwenyekiti wa Kamati ya Waamuzi ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Nassor Hamduni. **PICHA: FRANK MONYO**

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >